**Muuguzi** mbaroni tuhuma kumbaka mjamzito miezi 9

UKURASA 5



**Ripoti** yabaini rushwa ngono kikwazo zabuni kwa wanawake

UKURASA 19


Ukurasa 12

**Jumuiya Wazazi yatangaza ujenzi benki, hospitali kikanda**

Ukurasa 13

Katiba mpya kwa maslahi ya wote ni sahihi, lakini...

**siasa**

JUMATANO JUNI 14, 2023

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

Ukurasa 14

**Museveni shujaa harakati za 'no' ushoga, anapokwaa UVIKO-19**

**Chama ACT-Wazalendo chaona jambo Muungano, katiba yatakiwa kulimaliza**

• Chataja makuu ya Samia, haijawahi tokea tangu 1964

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

MAKAMU Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo, ambaye pia Makamu wa Kwanza wa Rais wa SMZ, Othman Masoud, anasema Zanzibar inahitaji mamlaka kamili ili kufunguka kiuchumi katika mfumo wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Anapohutubia mikutano ya ACT-Wazalendo, anasema mfumo wa sasa unainyima Zanzibar fursa ya kujiamulia mambo yake na kuwataka wananchi na viongozi wa Zanzibar kutumia fursa ya mchakato wa mabadiliko ya katiba kutetea mambo ya msingi yatakayonufaisha Zanzibar.

Aidha, anasema mchakato wa marekebisho ya katiba uliozishwa na Rais Samia ni fursa pekee ya kuondosha mambo yanayoikandamiza Zanzibar kiuchumi ndani ya muungano huo.

Othman anasema licha ya Rais Samia kutoa mabilioni ya fedha kwa ajili ya kupunguza makali ya UVIKO-19, vijana hawakuandaliwa kuitumia fursa hiyo.

Akizungumzia wazalishaji wa mazao ya chakula, anasema wameshindwa kunufaika na soko la sekta ya utalii kwa sababu serikali imeshindwa kuwawezesha ili kuinua uzalishaji wa mazao mbalimbali.

"Sekta ya utalii Zanzibar inategemea chakula kutoka Tanzania Bara kwa sababu wakulima wetu hawakuandaliwa lakini kama wangewezeshwa wangenufaika," anasema Othman.

Halikadhalika anasema asilimia 80 ya wafanyakazi katika sekta ya utalii wanatoka nje ya Zanzibar kwa sababu serikali haijawaandaa vijana wake kitaaluma tangu ilipoazishwa sekta hiyo na serikali ya awamu ya tano chini ya mstaafu Dk. Salmini Amaour Juma.

Othman anasema hatua hiyo ina madhara makubwa kwa sababu inasababisha mzunguko wa fedha Zanzibar kupungua na kusafirishwa nje wanakotoka wafanyakazi hao.

Ismail Jussa Ladhu, Mjumbe wa Kamati Kuu ya ACT- Wazalendo.

Anasema juhudi za kuondosha umasikini zinahitajika kwa vile vijana wingi Zanzibar wanakabiliwa na tatizo la ajira.

**SOKO HURIA KARAFUU**

Makamu huyo anaigeukia karafuu ambayo ni maarufu visiwani hapa akisema ni miongoni mwa mazao yanayochangia pato la taifa.

Anasema ACT-Wazalendo itaruhusu, soko huria kwa zao la karafuu muda mfupi watakaposhika madaraka kupitia uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 na kusema mfumo unaotumika hivi sasa mkulima kufanyakazi ya kuzalisha na serikali kuuza katika soko la nje si mwafaka na unachangia kurudisha nyuma maendeleo ya zao hilo.

Anasema historia inaonyesha Zanzibar ilikuwa inaongoza kwa uzalishaji wa karafuu kwa kuzalisha karibu tani 20,000 lakini uzalishaji umeshuka na kufikia tani kati ya 4,000 hadi 5,000.

Othman anasema hakuna njia nyingine ya kuendeleza karafuu zaidi ya zao hilo kuachiwa kuwa huria jambo ambalo litamaliza hata biashara ya magendo.

"Pamoja na serikali kufidia bei ya sasa kwa asilimia 80 wakulima bado kuna haja ya kuachiwa wenyewe wauze katika soko la nje badala ya wao kuwa wakulima na serikali kuwa wauzaji," anasema.

Anaeleza kuwa gharama za uzalishaji wa karafuu ni kubwa na kutoa mfano pishi moja au kilo moja lina faida ya Shilingi 7,800 ukitoa malipo ya mchumaji na mkulima katika pishi hilo mkulima anabakia na 4,000 mbali na gharama za matayarisho ya vifaa vya kukaushia karafuu.

Karafuu daraja la kwanza hivi sasa inauzwa Shilingi 14,000 kwa kilo ambapo serikali ya awamu ya saba chini ya uongozi wa Dk. Ali Muhamed Shein, ilipandisha bei ya zao hilo kutoka Shilingi 10,000 kwa daraja la kwanza na kufikia 14,000.

**SAMIA JUU ZAIDI**

Wakati Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ukielekea miaka 60 tangu kuazishwa mwaka 1964 ACT-Wazalendo, inasema Rais Samia Suluhu Hassan, amefanya jambo ambalo halijawahi kutokea katika historia ya muungano huo.

Ismail Jussa Ladhu, mjumbe wa Kamati Kuu ya ACT Wazalendo, anasema Rais Samia amepatia kiwango kikubwa cha mgao wa fedha za UVIKO-19 Zanzibar baada ya serikali kukopa katika Shirika la Fedha Duniani (IMF) ili kupunguza makali ya athari ya maradhi ya UVIKO-19 kwa taifa.

Jussa amekuwa akimwagia sifa Rais Samia kila anapohutubia mikutano ya hadhara ya chama hicho inayoendelea Zanzibar licha ya kuonyeshwa kukerwa na matumizi mabaya ya fedha hizo.

"Katika historia ya Muungano ni mara ya kwanza kupata mgao mkubwa wa fedha kama hizi ambazo Zanzibar imepatiwa bilioni 230 kwa ajili ya miradi ya maendeleo baada ya sekta za kiuchumi kuathiriwa na maradhi ya UVIKO-19," anasema Jussa.

Tanzania ilikopa Shilingi trilioni 1.3 kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF) ili kukabiliana na ugonjwa wa UVIKO-19 kuelekea mwishoni mwa mwaka 2021.

Anaeleza kuwa Rais anapambania kuiletea nchi maendeleo bila ya kuminya upande wowote wa Muungano ili kuhakikisha hali sawa kwa pande mbili hizo.

Aidha, anasema licha ya juhudi hizo za Rais Samia kutoa mgao wa fedha kuipatia Zanzibar lakini anasema kuna ubadhirifu mkubwa katika matumizi ya fedha hizo ambazo ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya SMZ na Serikali ya Muun-

INAENDELEA UK. 12

UKURASA 11

**Nipashe**

Jumatano Juni 14, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

ISSN 0856 • Na. 0581341

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US

# Samia azuia chakula kuuzwa nje ya nchi

## YALIYOMO

**UKURASA WA 4**

RIPOTI YA UCHUNGUZI-3

**DC AFUNGUKA SABABU OPERESHENI ASKARI- PORI DHIDI YA WANAKIJIJI**

JANA, sehemu ya pili ya ripoti hii inayotokana na ziara rasmi ya Nipashe katika eneo la tukio, ilianika madhila kutoka kwa wahusika...

**UKURASA WA 7**

**MSHTAKIWA KESI YA KULAWITI AGOMA KUJITETEA DAKIKA NANE**

MSHTAKIWA anayetuhumiwa kumlawiti mtoto wa miaka 12, Juma Rashid ametumia dakika nane kukataa kujitetea mbele ya...

**UKURASA WA 8**

**WAZIRI ATANGAZA MAZAO UTALII YANAYOPATIKANA TANZANIA PEKEE**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Mohamed Mchengerwa, ametangaza mazao rasmi matatu ya utalii ambayo hayapatikani nchi...

• **Ghala** la Taifa kuhifadhi tani 700,000, zaidi ya mara mbili na nusu ya mwaka jana... *Endelea ukurasa 2*




Rais Samia Suluhu Hassan akimsikiliza Askofu Mkuu Jimbo Kuu Katoliki la Mwanza, Renatus Nkwande, alipompa maelezo kuhusu Kituo cha Utamaduni na Makumbusho ya Wasukuma Bujora, baada ya kuwasili kituoni hapo, Magu mkoani Mwanza jana. **PICHA: IKULU**

## LHRC yataka mapitio ya mkataba Bandari

UKURASA 2

## Wadau habari waona nuru muswada wa sheria yao

UKURASA 3

**MICHEZO** **YANGA YATOA MSIMAMO, MAYELE, NABI** UK.24 **KATUNI** UK.6



Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Tanzania, Jenerali Jacob Mkunda (aliyeshika mkasi), akikata utepe kuashiria ufunguzi wa kituo cha mafuta cha SUMAJKT Energies kilichoko Mlalakuwa mkoani Dar es Salaam. **Habari ukurasa 3 PICHA: ROMANA MALLYA**

# Samia azuia chakula kuuzwa nje

**Na Vitus Audax,** MWANZA

RAIS Samia Suluhu Hassan amepiga marufuku uuzaji wa chakula nje ya nchi huku akiagiza kila Mtanzania kuhifadhi chakula, kwa ajili ya kukabiliana na uhaba wa chakula na mfumuko wa bei unaoendelea kupaa ulimwenguni kote.

Kiongozi huyo alitoa agizo hilo jana wakati akifungua Tamasha la Utamaduni la Sherehe za Mavuno, maarufu Bulabo, lililofanyika wilayani Magu mkoani Mwanza.

Alisema kuwa licha ya kuwapo mavuno makubwa nchini na kushuka kwa bei za chakula, bado hali ni ngumu ulimwenguni.

Alisema mfumuko wa bei umeendelea kuwa juu ya kiwango kilichotarajiwa kutoka asilimia tano hadi asilimia 10 na kwenda mbele kutokana na janga la UVIKO-19.

Rais Samia aliwataka Watanzania kuendelea kutumia sherehe hizo za mavuno kuwa waangalifu na kutunza akiba ya chakula, ili kukabiliana na mfumuko wa bei unaoendelea kupaa.

Alitaja jitihada za serikali katika kukabiliana na mfumuko huo wa bei kuwa ni pamoja na usajili wa wakulima, kutoa mbolea ya ruzuku kwa wananchi na kuwa tayari zimetengwa fedha kwa ajili ya kujenga skimu ya umwagiliaji kwa lengo la kulima na kuvuna mara mbili kwa mwaka.

Kadhalika, alisema wanatarajia kujenga maghala kila mkoa kwa lengo la kuhifadhi chakula kila mkoa sambamba na kuongeza thamani ya mazao yanayovunwa, ili yauzwe kwa bei kubwa na kumnufaisha mkulima.

"Kwa mwaka huu tutakuwa na hifadhi ya mazao tani 700,000 kwa ajili ya akiba ya dharura. Vilevile tunawataka wananchi sehemu zote kuhakikisha wanatunza chakula chao," alisema.

Kiwango cha chakula kinachotarajiwa kuhifadhiwa ni takribani mara mbili na nusu ya kiwango kilichohifadhiwa mwaka jana kwa mujibu wa taarifa za Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA).

Rais alieleza kuwa kwa sasa tani moja ya akiba inahudumia watu 500, lakini serikali inahitaji kurudi katika tani moja kuhudumia watu 20 pekee nje ya chakula cha akiba kilichopo katika ngazi ya familia.

Kuhusu kuimarisha utamaduni, Rais Samia aliwataka machifu nchini kuhakikisha wanalinda utamaduni na kurithisha kwa vijana na kuhakikisha wanadhibiti mmomonyoko wa maadili unaosababishwa na tamaduni za kigeni.

Akizungumza katika tamasha hilo, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Balozi Dk. Pindi Chana alionyesha kufurahishwa na hali ya urithishwaji wa sanaa na utamaduni kwa watoto hali inayoendelea kuimarisha tamaduni za nchini, huku akiwataka kusajili vikundi vyao ili wafikiwe kwa wakati na kupewa misaada pindi unapohitajika.



Mkurugenzi wa Kituo cha Bujora ambao ni waanzilishi wa tamasha hilo, Padri Ananias Fikili alisema lengo la sherehe hizo ni kusherehekea mavuno kwa Wasukuma.

Sherehe hizo zinajumuisha tamaduni za ngoma za asili ya Wasukuma pamoja na sherehe za maadhimisho ya Ekaristi Takatifu kwa Kanisa Katoliki, lengo likiwa ni kufikisha injili kupitia tamaduni.

**UTEUZI**

Katika hatua nyingine, Rais Samia amefanya uteuzi wa viongozi watatu kuwa na hadhi ya ubalozi ambao ni Katibu Mkuu Kiongozi, Dk. Moses Kusiluka, Dk. Salim Hamad ambaye ni Msaidizi wa Rais anayeshughulikia masuala ya siasa na Msaidizi wa Rais anayeshughulikia masuala ya hotuba, Dk. Kassim Khamis.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa jana, uteuzi huo wa hadhi ya balozi ulianza Juni 12, mwaka huu, na vyeo walivyonavyo vinabaki kama vilivyo, na wateule wataapishwa Juni 16 mwaka huu, Ikulu ya Chamwino, Dodoma.

Rais pia amemteua aliyekuwa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Rogatus Mativila kuwa Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI (Miundombinu).

Pia amemteua Mohamed Besta kuwa Mtendaji Mkuu wa TANROADS. Kabla ya uteuzi, alikuwa Mkurugenzi wa Ufundi wa Wakala wa Usimamizi wa Usalama wa Usafiri wa Anga wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (CASSOA).

Rais Samia pia amemteua Kamishna Benedict Wakulyamba kuwa Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Maliasili na Utalii, akichukua nafasi ya Anderson Mutatembwa aliyehamishiwa kuwa Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu).

Katika uteuzi huo ambao umeanza Juni, 12, mwaka huu, Rais pia amemteua Mhandisi Amin Nathaniel Mcharo kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya TANROADS.

# LHRC yataka mapitio mkataba Bandari

**Enock Charles na Mary Geofrey**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kimeishauri serikali kurejea upya vipengele vya mkataba wa ushirikiano wa kiuchumi na kijamii kwa ajili ya uendelezaji na uboreshaji wa utendaji kazi wa bandari kati ya Serikali ya Tanzania na Dubai.

Kimesema lengo ni kuwekwa wazi baadhi ya vipengele muhimu, ikiwamo kiwango cha umiliki, faida itakayopatikana na muda wa uwekezaji.

Ushauri huo ulitolewa jana kwa nyakati tofauti jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi wa LHRC, Dk. Anna Henga na Balozi Dk. Slaa walipozungumza na waandishi wa habari. Walizingatia Ibara ya 18(2) ya Katiba ya nchi.

Dk. Anna alisema upo umuhimu wa kuwekwa wazi kwa vipengele hivyo katika mkataba mkubwa, ili kuondoa hofu iliyopo kwa wananchi badala ya kusubiri kuviweka vipengele hivyo katika mikataba ya utekelezaji ambayo itategemea ubora wa mkataba mkubwa.

"Mkataba mkubwa ni kama Katiba, Katiba ikiwa mbovu, hata sheria zinafuata haziwezi kuwa nzuri, mkataba mkubwa ukiwa na matatizo hata mikataba ya utekelezaji haiwezi kuwa na ubora unaotakiwa na wanaweza wasiweke vipengele hivyo kwa kuwa havijatajwa kwenye mkataba mkubwa.

"Mkataba haujaweka wazi, faida ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itapata baada ya kuanza utekelezaji wa mkataba huo, jambo hili linaongeza hofu ya kuingia mkataba huu kwa kuwa hakuna mahali ndani ya mkataba unapoonyesha matarajio ya faida itakayopatikana kila mwaka kwa serikali na thamani ya jumla ya utekelezaji wa mkataba huo," alisema.

Kuhusu ukomo wa mkataba, mkurugenzi huyo alisema mkataba haujawekwa muda mahususi wa utekelezaji wa mkataba huo kama ilivyo misingi inayoongoza uendeshaji wa mikataba ya kimataifa, moja ya msingi huo akisema ni muda wa ukomo wa mkataba.

Alisema ni muhimu kuwapo kwa kipindi maalum cha ukomo wa mikataba ya utekelezaji ili kutoingia katika utata wa kisheria uliopo katika ibara ya 23 ya mkataba huo ambayo haiko bayana kuhusu ukomo wa mkataba badala yake inaweka mazingira yatakayopelekea kukoma kwa mkataba, ikiwamo kusitishwa kabisa kwa miradi yote ya kimkataba pamoja na kuisha kwa mikataba ya utekelezaji wa miradi.

"Hata hivyo, ibara ya 23 (2) inaweka sharti la kuendelea kwa mkataba hata baada ya kusitishwa kwa mkataba huo kwa hoja ya kuwa mkataba umesitishwa nje ya muda. Hivyo ni wazi kwamba mkataba umeweka masharti magumu ya usitishwaji wake," alisema.

Kuhusu utatuzi wa migogoro, alisema kipengele cha utatuzi wa migogoro kilichopo katika ibara ya 20 (2) (e) kinapingana na kifungu cha 11 cha Sheria ya Ulinzi wa Rasilimali za Umma Na. 5 ya mwaka 2017 kinachotaka migogoro yote ya uwekezaji isikilizwe na Mahakama ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika mkataba huo endepo kutatokea mgogoro utatatuliwa na vyombo vya usuluhishi wa migogoro Johannesburg, Afrika Kusini.

Kuhusu motisha za kikodi, mkurugenzi huyo alisema ibara ya 9 na 18 vinaainisha masuala ya kikodi, ushuru wa forodha na makato mengine yatakayofanywa kwa mujibu wa sheria, lakini kipengele hicho kinatoa mwanya kwa serikali kutoa motisha kwa mwekezaji wakati mkataba hautaji aina au kiwango cha motisha, hivyo kituo kinapendekeza mikataba ya utekelezaji iainishe ukomo wa juu na wa chini wa motisha hizo zitakazotolewa katika mikataba mingine ya utekelezaji.

Alisema lengo ni kuepuka kutumika vibaya kwa kipengele hicho kwa baadhi ya watendaji wa serikali wasio waaminifu kwa kuwa wanaweza kutoa misamaha ya kodi na nafuu nyingine kwa kadri wanavyoona inafaa.

Kuhusu sharti la mwekezaji kutoingiliwa, alisema ibara ya 6 inaweka takwa la serikali kuhakikisha kampuni ya uwekezaji inapata vibali haki ya kutumia ardhi na motisha za kiuwekezaji kwa ajili ya utekelezaji wa mkataba.

# Wadau habari waona nuru muswada wao

Na Jenifer Gilla

WADAU wa habari wameeleza kuridhishwa na marekebisho ya Sheria ya Huduma za Habari, 2016, wakitaka marekebisho katika vifungu vingine vinavyohitaji kuangaliwa ili kuifanya taaluma ya habari kuendelea kustawi vyema.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, wadau hao akiwamo Makamu Mwenyekiti wa Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika, Tawi la Tanzania (MISA Tanzania), James Marenga, walisema amefurahi kuona baadhi ya vipengele vimefanyiwa marekebisho ingawa hawajaridhishwa na kitendo cha kamati kupeleka bungeni baadhi ya marekebisho na kuacha mengine.

Alisema walipeleka kwa Kamati ya Bunge mapendekezo 21 lakini machache yamepelekwa bungeni huku tisa yakifanyiwa marekebisho ambayo kati ya hayo matatu ndio anaona yenye msingi ikiwamo kifungu namba tano, 38, 50 hadi 55 na 63 hadi 64.

Alitaja moja ya mapendekezo waliyoyatoa ambayo hayajapelekwa bungeni ni muundo wa vyombo vinavyoundwa na sheria hiyo ikiwamo baraza huru la habari.

Mjumbe wa Kamati Tendaji ya Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Neville Meena, alisema kuna mambo mengi waliomba yafanyiwe kazi lakini hayafanyiwa ikiwamo msajili kusajili leseni kila mwaka kwa kuwa inaleta shida kwa vyombo vya habari kwa kuwa kuna viongozi wanatumia hiyo nafasi vibaya.

Alipongeza kuondolewa kifungu namba tano ambacho kinapendekeza kufanyiwa marekebisho kwa lengo la kumwondolewa Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Habari jukumu la uratibu wa matangazo yote ya serikali.

**MAREKEBISHO**

Katika marekebisho hayo yaliyojadiliwa bungeni jana, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alisema kati ya hoja 21 walizopokea kutoka kwa wadau, walikubaliana kuwa hoja tisa zifanyiwe marekebisho ikiwamo kuondoa kabisa kifungu 38(3) cha Sheria ya Huduma za Habari kilichoweka masharti ya mtu kushtakiwa kwa makosa ya kijinai.

Nape alisema pia walikubaliana mapendekezo manane yabaki kama yalivyo katika sheria na baadhi ya mambo ikiwamo muda wa umiliki wa leseni.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Jaji Ezekiel Feleshi, alisema serikali imepiga hatua kubwa katika maboresho ya sheria hiyo, tangu ilipotungwa mwaka 2016 kwa kuwa ililenga kuifanya huduma ya habari kuwa ya kitaaluma, ikiwamo kuweka bodi na baraza ambalo wajumbe wake ni wanahabari.

Alisema pia makosa yanayohusiana na kazi za habari yamepunguzwa ikiwamo faini ambayo sasa ni kuanzia Sh. milioni 3 hadi milioni 10 ambapo awali ilikuwa ni Sh. milioni tano hadi milioni 20, huku kifungo kikirekebishwa kufukia miaka miwili mpaka mitano kutoka miaka mitatu hadi mitano.

# Mkuu JKT ataka ubunifu miradi ya maendeleo

Na Romana Mallya

MKUU wa Majeshi ya Ulinzi Tanzania, Jenerali Jacob Mkunda, amelitaka Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) wakati likijiandaa kuadhimisha 60, lijitathmini kubuni miradi mikubwa ya kimkakati itakayoendana na Dira ya Taifa.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa kituo cha mafuta cha Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT) kilichojengwa maeneo ya Mlalakuwa mkoani Dar es Salaam, kikiwa ni miongoni mwa miradi inayofanywa na shirika hilo.

Kituo hicho ambacho kinajulikana kama SUMAJKT Energies ni miongoni mwa vituo vya mafuta ambavyo shirika limepanga kuvijenga kwenye majiji yakiwamo Arusha, Dodoma, Mbeya na Tanga.

"Julai Mosi, mwaka huu, JKT litaadhimisha miaka 60 hiki ni kipindi kifupi, na jeshi limefanya mambo mengi na makubwa. Mradi kituo hiki cha mafuta ni mojawapo ya miradi mingi ya JKT chini ya SUMAJKT.

"Miradi ndiyo namna sahihi ya kuongeza uwezo wa kujitegemea, ni darasa muhimu kwa vijana ili kuwafanya wawe wabunifu na kuwa na uzoefu wa kuiendesha. Inawaandaa vijana kujitegemea na kuwa na kuongeza kiwango cha uzalendo wa kuilinda nchi," alisema.

Kiongozi huyo alisema wakati wakielekea miaka 60, anaamini umefika wa kuanza kubuni miradi mikubwa ya kimkakati ambayo lengo lake litakuwa ni kuimarisha ulinzi wa nchi.

"Tufikirie kuanzisha miradi mikubwa ya kimkakati itakayoendana na dira ya taifa. Ninatambua Jeshi la Kujenga Taifa ndio kazi yenu mmekuwa mkifanya miradi mingi, nina wahasa mfanye miradi mingine mikubwa zaidi," alisema.

Aliwataka waendelee kuanzisha vituo vya mafuta kila mahali kwa kuwa SUMAJKT ndiyo kinara wa kubuni miradi.

Mkuu wa JKT, Jenerali Rajab Mabele alisema kituo hicho ni moja ya maelekezo yake na kwamba, wamejipanga wawe na vituo kama hivyo kwenye majiji yote.

Mkurugenzi Mtendaji wa SUMAJKT, Kanali Petro Ngata, alisema shirika kwa kutambua malengo ya kuanzishwa kwake, ambayo ni kuchangia uwezeshaji wa shughuli za JKT na kujenga uchumi wa taifa limeamua kuwekeza kwa kujenga kituo hicho cha mafuta.

Wakati huo huo, Mkuu wa Tawi wa Utawala JKT, Brigedia Jenerali Hassan Mabena, amesema wanatangaza kusitisha kupokea vijana wa JKT kwa mujibu wa Sheria ya mwaka 2023.

"Vijana ambao walishindwa kuripoti kwa muda waliopangiwa hawatapokewa kambini, hivyo wasiende kuripoti. Jeshi lilitoa wito kwa vijana wote waliohitimu elimu ya kidato cha sita kwa mwaka 2023 kutoka shule zote Tanzania Bara kuhudhuria kambi walizopangwa.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS,
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA
MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO

TANGAZO LA MNADA WA HADHARA WA VIFAA CHAKAVU

Wananchi wote mnatangaziwa kuwa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) itauza kwa njia ya mnada wa hadhara wa vifaa chakavu yakiwemo magari, samani za ofisi pamoja na vifaa vingine siku ya Jumanne tarehe 27 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dar es Salaam na Alhamisi tarehe 29 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dodoma.

Wananchi wote watakaoshiriki mnada huo wanaombwa kufika siku ya Jumapili tarehe 25 Juni, 2023 katika Jengo la UTUMISHI Kivukoni Dar es Salaam kwa ajili ya ukaguzi wa vifaa hivyo ambavyo ni viti vya ofisini "Office Chairs", "Printers" na "Laptops" na siku ya Jumanne tarehe 27 Juni, 2023 kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni katika Ofisi za e-GA Mji wa Serikali Mtumba Dodoma kwa ajili ya ukaguzi wa vifaa hivyo, ambapo pamoja na vifaa vingine, magari yote yameegeshwa katika ofisi za e-GA.

**Maelezo zaidi ya magari hayo ni kama yanavyoonekana katika jedwali:**

| Na | Aina | Modeli | Namba ya Usajili | Mahali lilipo | Hali ya Gari |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | TOYOTA station wagon Diesel Engine | LAND CRUISER V8 | STL2039 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |
| 2 | Mitsubishi Pajero 4WD, Station Wagon with 2.8L Diesel Engine, | PAJERO ST WAGON | STL2011 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |
| 3 | Mitsubishi Pajero 4WD, Station Wagon with 2.8L Diesel Engine | PAJERO ST WAGON | STL2010 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Magari hayajalipiwa ushuru na kodi ya ongezeko la thamani (VAT), hivyo Mnunuzi atatakiwa kulipa ushuru na kodi zingine kabla ya kulichukua toka Mamlaka ya Serikali Mtandao
2. Magari yatauzwa kama yalivyo mahali yalipo
3. Mnunuzi wa gari atalazimika kulipa papo hapo amana "deposit" isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya gari na atakamilisha malipo yote ndani ya muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hilo atakosa haki zote za ununuzi wa gari na amana iliyolipwa haitarudishwa.
4. Mnunuzi wa gari atatakiwa kuondosha au kuchukua gari ndani ya muda wa siku saba (07) kuanzia siku ya kukamilisha malipo.
5. Ruhusa ya kuangalia gari itatolewa kwa siku mbili (02) kabla ya tarehe ya mnada husika.
6. Kwa Mnunuzi wa vifaa vingine atatakiwa kulipia kifaa alichopata baada tu ya kumtangaza dalali kuwa mshindi (on fall of the hammer). Kifaa ambacho hakijalipiwa kitanadiwa upya. Pia mnunuzi atakiwa kuchukua kifaa alichonunua papo hapo mara tu baada ya kulipia (cash and carry)
7. Mnada utaanza saa nne (4:00) asubuhi siku ya Jumanne tarehe 27 Juni katika ofisi zake za Dar es Salaam, 2023 na Alhamisi tarehe 29 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dodoma.

**Imetolewa na**
**Mkurugenzi Mkuu**
**Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)**

Mji wa Serikali, Mtaa wa Mtandao, S. L. P. 2833, Dodoma, Simu: +255222129868, Nukushi: +255222129878,
Barua Pepe: info@ega.go.tz, Mkurugenzi Mkuu: dg@ega.go.tz, Tovuti: www.ega.go.tz
"Uadilifu na Ubunifu kwa Utoaji Huduma Bora kwa Umma"

The Guardian
The Home of Great Newspaper
Our Regional Offices and Representatives




*Feel free to contact for:*
ADVERTISEMENT ON NEWSPAPERS / DIGITAL PLATFORMS AND SUBSCRIBING NEWSPAPERS / E-PAPERS

HEAD OFFICE
THE GUARDIAN LIMITED
MIKOCHENI AREA
P.o.Box 31042, Dar es salaam, Tanzania
Tel: + 255 745700710 | Email: info@guardian.co.tz

Nipashe @Nipashetz
The Guardian @Theguardiantz
IPP media

**RIPOTI YA UCHUNGUZI - 3**

MKASA ASKARI-PORI KUDHURU MBARALI...

# DC afunguka sababu zake kuhalalisha operesheni askari dhidi ya wanakijiji

**Na Halfani Chusi, aliyekuwa**
MBARALI

***JANA, sehemu ya pili ya ripoti hii inayotokana na ziara rasmi ya Nipashe katika eneo la tukio, ilianika madhila kutoka kwa wahusika, maelezo ya mwenyeji mkazi tangu zama za miaka ya 1950, mamlaka za uongozi kijijini, zikikiri na kufafanua undani wa matukio. Endelea na sehemu ya mwisho.***

Safari ya Nipashe baada ya kupata undani kutoka kijijini, ikahamia ofisini kwa Mkuu wa Wilaya Mbarali, Kanali Denis Mwila, anayekiri kufahamu mgogoro huo kati ya wafugaji na askari wa TANAPA, ambao anawatetea kwa kauli "wafugaji hao wako ndani ya hifadhi, lazima nguvu itumike kuwahamisha!"

Huku akiongea kwa ukali, Kanali Mwila anawataja wafugaji ni wakorofi, huku akiwa na ufafanuzi kwamba wote walikutwa hifadhini wakilisha mifugo yao, tabia ambayo pia wanawafanyia majirani zao, wakulima.

"Lakini kubwa zaidi, wale ni wakorofi. Waliwahi kuwaua askari wetu wawili wa TANAPA. Kwa hiyo, wale sio wapole kama watu wanavyodhani.

"Kibaya zaidi, wamewakaribisha wafugaji kutoka maeneo mengine, kwa hiyo kilichopo mifugo imekuwa mingi kuliko mahitaji ya eneo.

"Tunachotaka hapa ni kuushirikisha uongozi wa mkoa kupunguza ng'ombe wao kwa sababu hawana faida yoyote kwetu, kwa sababu wanaharibu mazingira pamoja na ikolojia ya hifadhi," anatamka Kanali Mwila.

Anasema kasoro nyingine za ikolojia zinazosababishwa na shughuli hizo za ufugaji, ni kuathiri mtiririko wa maji Mto Ruaha, ambako ni chanzo cha maji ya umeme kitaifa.

Hapo Kanali Mwila anafafanua: "Sisi hatulindi hifadhi ile kwa ajili ya maslahi yetu hapana! Tunalinda kwa ajili ya maslahi ya nchi nzima. Ukiona nchi ina tatizo la maji na umeme, ujue chanzo ni hapa."

Kanali Mwila, ambaye ufafanuzi wake ulibebwa zaidi na lafudhi ya kiaskari na sentensi nzito 'zilizovuka mipaka', anawanyooshea kidole viongozi wa kisiasa na anaowataja kuwa 'wakubwa serikalini', akidai wako nyuma ya mgogoro huo na 'wanatumia mwanya huo kujisafisha'.

"Sisi hatupo hapa kuangalia maslahi ya chama fulani, tupo hapa kuhakikisha tunaisimamia hifadhi, kwa maslahi ya Taifa letu," anatamka.

Katika ufafanuzi wake huo, anatumia lugha ya fasihi, akisema wao mamlaka ya kiserikali wanafanana na kinyonga ambaye anapotaka kuzaa, hupanda juu ya mti kisha anadondoka chini anakufa, watoto wanazaliwa, na ndio staili aliyoamua kuitumia kuilinda hifadhi hiyo.



Kanali Mwila, Mkuu wa Wilaya ya Mbarali



Dk. Anna Henga, Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC

Katika ufafanuzi wake ambao hakuipatia Nipashe ushahidi, Kanali Mwila anadai mgogoro huo ndani yake kuna viongozi anaowataja wa ngazi ya chini wananufaika kwa rushwa, ili watoe taarifa zinazozua taharuki, fedha hizo akizitaja 'zinazoweka kufika Sh. milioni 300', zinatolewa na wafugaji ili kuhitimisha maslahi yao.

Anadai nyuma ya pazia, kinachowavutia wafugaji kung'ang'ania eneo hilo kwa hali yoyote ile kwamba ni ardhi yenye majani yenye rutuba na chumvichumvi, ambayo ni lishe chanya kwa afya ya ng'ombe, akinena:

"(Ng'ombe) anapokula ananenepa sana, na mbuzi pia wanazaa hadi mara tatu kwa mwaka, ndio maana wamekuwa wagumu kuondoka eneo lile kwa hiari."

Hata hivyo, katika hoja inayokinzana na msimamo wake katika utambulisho, akaahidi askari wanaodaiwa kutenda kosa, walishakamatwa kwa ajili ya uchunguzi wa kisheria.

**UTATA MKAZI 1953**

Kanali Mwila anapinga uwezekano wa kuwapo mkazi wa kijiji chenye mgogoro, tangu mwaka 1953, akitumia vigezo vya ushahidi kwamba:

"Wanaosema wapo hapa tangu mwaka 1953, ukiangalia hata nyumba wanazokaa hazifanani na huo muda. Eneo lile linatambulika kama hifadhi tangu mwaka 1910, hata hivyo wamekaa kwa muda huo wote kwa huruma ya serikali."



Baadhi ya wanakijiji wanaodai kudhalilishwa na askari-pori wa Hifadhi ya Taifa Ruaha wilayani Mbarali hivi karibuni. **PICHA: HALFANI CHUSI**

**ANAVYOSAKA SULUHU**

Mkuu wa Wilaya huyo, anataja hatua wanazochukua zinajumuisha kutoa elimu kwa wakazi kuhusu umuhimu wa uhifadhi na Mto Ruaha unaopita jirani nao, wakitumia mbinu shirikishi.

Anataja hatua nyingine iliyopo sasa, wanafanya uthamini kwa ajili ya kuandaa malipo, wanakijiji wahame, akisema ni jambo linalofahamika na kuna vijiji vimesharidhia.

Kuhusu sakata la aliyeporwa ng'ombe 170 na fedha Sh. milioni 17, Kanali Mwila anakiri kulifahamu na aliopomwita mhusika ofisini kwake, hakuwa na ushahidi kuthibitisha madai yake.

"Alikuja hapa ofisini kwangu, ili nione namna ya kumsaidia. Nikamwambia leta risiti ya benki inayoonyesha kama ulitoa hizo pesa, hana! Nikamwambia 'mimi ninashindwa namna ya kukusaidia kwa sababu siwezi kuthibitisha kama kweli ulikuwa na hao ng'ombe'.

"Nikamwambia leta namba ya usajili wa ng'ombe wako, tujue walikuwa wangapi, nayo hana! Nikaona malalamiko yake hayana mashiko. Nikamwambia kama anaona mimi nimeshindwa, kumsaidia aende mahakamani akafungue kesi," anaeleza.

Kuhusu waliodai kuteswa wakiwa uchi, Kanali Mwila anadai ni jambo la kisiasa aliloliibua mbunge bungeni na halina ukweli wowote. Anayataja ni mambo ya kufikirika.

Hata hivyo, Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Michael Semindu, anakiri kuwa na taarifa za askari-pori kuwapiga wafugaji, akisisitiza ni vitendo vinavyokiuka haki za binadamu na sheria ya nchi na alishawaonya na kuwataka kutorudia kutenda unyama huo.

Anasema ili kuepukana na migogoro hiyo, tayari serikali imetenga eneo lenye ukubwa wa ekari 932 kwa ajili ya wanakijiji ambao watatolewa hifadhini. Watahamishiwa katika vijiji 10. Utekelezaji utafanyika baada ya msimu huu wa kilimo kufika ukomo.

Mkazi wa Mbarali, pia Mbunge wa Viti Maalum, Bahati Ndingo, anasema kitendo kilichofanywa na askari-pori ni kinyume cha sheria. Walipaswa kuwakamata watuhumiwa na kuwafikisha polisi au mahakamani kwa ajili ya hatua za kisheria.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, anakiri kuwa kupokea taarifa ya matukio ya ukatili huo wa askari-pori dhidi ya wanakijiji. Alishaagiza waliotenda tukio hilo kukamatwa na kufanyike uchunguzi wa kina kisha hatua za kisheria zichukuliwe ikiwamo kufikishwa mahakamani huku akiwazuia wafugaji kuendeleza makazi mapya hifadhini.

Wakili wa Kujitegemea, Rose Omuga, anasema kifungu cha 15 cha Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori kinazuia mtu kuingia hifadhini isipokuwa kwa kibali cha mamlaka husika. Kwa kukiuka sheria hiyo, adhabu yake faini isiyopungua Sh. 100,000 na isiyozidi Sh. 500,000 au kifungo cha muda usiopungua mwaka mmoja na usiozidi mitatu gerezani.

Wakili huyo pia anasema kuingiza mifugo hifadhini ni kosa kisheria kulingana na sheria za hifadhi. Mifugo inapokutwa hifadhini, hatua zinachukuliwa kwa kuzingatia kifungu cha 21 cha Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura 283, kinachotoa katazo la mtu yeyote kulisha mifugo hifadhini.

"Adhabu yake ni faini isiyopungua Sh. 100,000 na isiyozidi Sh. 500,000 au kifungo cha gerezani kisichopungua mwaka mmoja lakini kisichozidi miaka mitano, au vyote kwa pamoja.

"Kwa hiyo, askari wa TANAPA walipaswa kuwapiga faini au kuwapeleka mahakamani kwa ajili ya kifungo, hivyo kwa kitendo cha kuwapiga, walitenda kosa kwa muujibu wa sheria," anafafanua.

Ni hoja inayoungwa mkono na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kupitia Mkurugenzi Mtendaji wake, Dk. Anna Henga, anayesema kitendo cha askari kuwatesa wafugaji hifadhini ni uvunjifu wa haki za binadamu.

Dk. Anna anasema askari hao hawakupaswa kuwapiga wanakijiji, bali walitakiwa kuwafikisha katika vyombo vya sheria, hivyo askari hao wawajibishwe kwa mujibu wa sheria za nchi.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Mohamed Mchengerwa, akizungumzia suala hilo baada ya kuzuru Mbarali wiki mbili zilizopita, aliagiza hatua zichukuliwe dhidi ya askari waliotenda ukatili huo huku akibainisha kuwa serikali itamega hekta 34,000 za hifadhi na kuzikabidhi kwa wananchi Mbarali.

# Muuguzi mbaroni tuhuma kubaka mjamzito miezi 9

**Na Halima Ikunji,** SIKONGE

MUUGUZI Msaidizi Daraja II wa Hospitali ya Wilaya ya Sikonge mkoani Tabora, Rayson Duwe, anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kumbaka magonjwa mwenye ujauzito aliyekuwa amelazwa hospitalini hapo kwa ajili ya matibabu.

Muuguzi huyo anadaiwa kumchoma sindano ya dawa za usingizi mama huyo mwenye ujauzito wa miezi tisa kisha kumfanyia ukatili huo, Kamanda wa Polisi mkoani Tabora, Richard Abwao, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo jana.

Alisema mjamzito huyo alifikishwa hospitalini huko Juni 9, mwaka huu saa mbili usiku akiwa anasumbuliwa na malaria na alilazwa kwa ajili ya matibabu zaidi.

Kamanda huyo alieleza kuwa uchunguzi wa awali unaonyesha mtumishi huyo aliyekuwa zamu siku hiyo, alikuwa eneo la mapokezi ya wagonjwa wa nje (OPD) na aliingia kazini akiwa amelewa.

Kamanda alifafanua kuwa mtuhumiwa akiwa na jukumu la kupokea wagonjwa, alitoka na kwenda chumba cha mgonjwa huyo na kumfanyia kitendo hicho.

Aliongeza kuwa mtuhumiwa alikutwa na wenzake akiwa chumbani humo na pembeni yake kulikuwa na vifaa vilivyotumika kumchoma mjamzito huyo dawa ya usingizi ijulikanayo kwa jina la Diazepam Injection ambayo ilimfanya kupata usingizi.

Aliongeza kuwa uchunguzi wa tukio hilo tayari umekamilika kwa ajili ya mtuhumiwa kupandishwa kizimbani ili kujibu tuhuma zinazomkabili.

Akizungumzia tukio hilo, Mkuu wa Wilaya hiyo, Simon Chacha, alisema hatua ya awali waliyochukua ni kumsimamisha kazi huku vyombo vingine vya sheria vikiendelea na taratibu zake.

Aliwataka watumishi wa umma wote katika halmashauri hiyo kufanya kazi kwa uadilifu na kwa mujibu wa viapo vya taaluma zao na kuonya kuwa yeyote atakayekiuka maadili ya kazi yake hawatosita kuchukua hatua.


## UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

TANESCO

## TANZANIA ELECTRIC SUPPLY CO. LTD

# RE-ADVERTISEMENT OF
## REQUEST FOR EXPRESSION OF INTEREST FOR CONSULTING SERVICES

## 87.8 MW KAKONO HYDROPOWER PROJECT
## Tender No. PA/001/2022-2023/HQ/C/05

## CONSULTANCY SERVICES FOR CONSTRUCTION SUPERVISION AND MANAGEMENT OF THE 87.8 MW KAKONO HYDROPOWER PROJECT IN KAGERA REGION

**Sector: Energy**
The Government of the United Republic of Tanzania has received financing from the African Development Bank (AfDB), French Development Agency (AFD) and the European Union (EU) towards cost of the 87.8MW Kakono Hydropower Project (HPP), and intends to apply part of the agreed amount to payments under the contract for "consultancy services for construction supervision and management of Kakono HPP in Kagera Region" in the north western part of Tanzania.

**The services under this project will entirely include and not limited to the following:**

a) Design review of existing feasibility study reports and prepare the associated works bidding documents,
b) Support the client in the procurement of works pertaining to the Kakono HPP,
c) Construction supervision of works comprising:
   i. 87.8 MW Kakono hydropower plant and associated facilities,
   ii. 38.5 km 220 kV evacuation transmission line from the power plant switchyard to the existing Kyaka 132/33 kV substation,
   iii. Uprating the existing substation from 132/33 kV to 220/132/33 kV.

In line with the International Commission on Large Dams, the construction supervision services will be conducted in collaboration with an independent panel of experts. The panel of experts, that is to be recruited separately, will provide support and guidance to the Project Implementation Team on matters pertaining to the construction of the hydropower plant in accordance with international best practices.

The Tanzania Electric Supply Company Limited (TANESCO), the client, now invites eligible consultants to indicate their interest in providing these services. Interested Consultants must provide information indicating that they are qualified to perform the services (brochures, description of similar assignments, experience in similar conditions, availability of appropriate skills among staff, etc.).

**Consultants may constitute joint ventures to enhance their chances of qualification.**
Eligibility criteria, establishment of the short-list and the selection procedure shall be in accordance with the African Development Bank's **"Procurement Policy for Bank Group Funded Operations"** dated October 2015, which is available on the Bank's website at **http://www.afdb.org.**

Interested consultants may obtain further information at the address below during office hours 09.00 – 12.30 hours and 14.00 – 16.30 hours, East African Time, (Monday to Friday) excluding public holidays.

Expressions of Interest must be delivered to the address below during office hours no later than **21st July, 2023 at 10:30 Hrs East African Time.**

Alternatively, the Expressions of Interest (either unzipped or zipped WINRAR or Winzap shall not exceed 15 MB) may be submitted online via the email **sec.tenderboard@tanesco.co.tz,** and the password shared via **pmuprojects@tanesco.co.tz.**

**Attn: The Secretary-Tender Board,**
**TANESCO Umeme Park Building, Ubungo,**
**Ground Floor, Tender Room, Room No. G04,**
**P.O. Box 9024,**
**Dar Es Salaam, Tanzania.**
**Tel: 255 (22) 2451145/2452172; +(255) 782 376147**
**Email: sec.tenderboard@tanesco.co.tz**
**pmuprojects@tanesco.co.tz;**

**Managing Director,**
**Tanzania Electric Supply Company Limited (TANESCO)**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Marufuku ya Rais kuuza chakula nje ya nchi imekuja wakati mwafaka

**JANA** Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa mkoani Mwanza alitahadharisha hatari ya wakulima kuuza chakula nje ya nchi na kupiga marufuku ili kujiepusha na mfumuko wa bei na kukabiliana na baa la njaa.

Wafanyabiashara kutoka nchi jirani wamekuwa na tabia ya kuwafuata wakulima kwenye mashamba yao na kuwarubuni kuwauzia mazao yakiwa bado shambani.

Wafanyabiashara hao wamekuwa wakiongeza fedha kidogo ili kuwashawishi wakulima hao na matokeo yake huingia kwenye mtego na kuuza mpaka akiba yao.

Akipiga marufuku hiyo, Rais Samia aliwataka wakulima wote wanaouza mazao yao nje ya nchi kuacha na kuwataka kuhifadhi chakula chao ili kukabiliana na baa la njaa pamoja na mfumuko wa bei unaoendelea kupaa ulimwenguni kote.

Wakati akifungua Tamasha la Utamaduni la sherehe za mavuno Bulabo, lililofanyika wilayani Magu mkoani Mwanza alisema kuwa licha ya kuwapo kwa mavuno makubwa nchini na kushuka kwa bei za chakula bado hali ni ngumu ulimwenguni.

Mfumuko wa bei umeendelea kuwa juu ya kiwango kilichotarajiwa kutoka asilimia tano hadi asilimia kumi na kwenda mbele kutokana na janga la UVIKO-19. Rais Samia alihadharisha.

Pia amewataka Watanzania kuendelea kutumia sherehe hizo za mavuno kuwa waangalifu na kutunza akiba ya chakula ili kukabiliana na mfumuko wa bei ambao hauiathiri Tanzania pekee, bali hata nchi nyingine duniani.

Alitaja jitihada za serikali katika kukabiliana na mfumuko huo wa bei kuwa ni pamoja na usajili wa wakulima, kutoa mbolea ya ruzuku kwa wananchi na kuhakikisha kuwa tayari zimetengwa fedha kwa ajili ya kujenga skimu ya umwagiliaji lengo likiwa ni kulima na kuvuna mara mbili kwa mwaka.

Kadhalika, serikali inatarajia kufanya ujenzi wa maghala kila mkoa kwa lengo la kuhifadhi chakula katika kila mkoa na kuongeza thamani ya mazao yanayovunwa ili yaweze kuuzwa kwa bei kubwa na kumnufaisha mkulima.

"Kwa mwaka huu tutakuwa na hifadhi ya mazao tani laki saba kwa ajili ya akiba ya dharura vilevile tunawataka wananchi sehemu zote kuhakikisha wanatunza chakula chao," Rais Samia anasisitiza.

Kwa sasa tani moja ya akiba inahudumia watu 500, lakini serikali inahitaji kurudi katika tani moja kuhudumia watu 20 pekee nje ya chakula cha akiba kilichopo katika ngazi ya familia.

Watanzania kwa ujumla lazima wazingatie umuhimu wa kuhifadhi chakula ili nchi isiingie katika janga la njaa.

Tumeshuhudia katika nchi mbalimbali jinsi wananchi wake wanavyokabiliana na tatizo la ukosefu wa chakula kiasi kinachoathiri pia wanyama wanaowafuga.

Ukosefu wa chakula katika nchi husababisha athari nyingi hivyo, tusikubali janga hilo liingie nchini.

Tanzania ina ardhi ya kutosha ya watu kulima na kupata chakula kingi ambacho kinaweza kutosheleza nchi na kubaki ziada.

Lazima wananchi waangalie maslahi ya nchi yao badala ya kufikiria kuuza chakula chote na baadaye kuilazimu serikali kuanza kuhaha kuagiza chakula hicho kutoka nje ya nchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Pilly Kigome

# Chonde chonde tuchangie damu

**KUHIMIZA** Watanzania kuchangia damu sasa, mara kwa mara na kila wakati ni kauli mbiu ya kitaifa ya mwaka huu, katika maadhimisho ya Siku ya Uchangiaji Damu Salama.

Ni sehemu ya juhudi ya kutetea uhai na kuokoa maisha ya wananchi hasa wagonjwa kuanzia wajawazito, wazazi, watoto na wanaopata ajali.

Ni kauli mbiu inayoamsha hisia, inayoonekana kuwa ya kizalendo na ya kihekima kwani imekuwa ina mtaka kila mmoja kuguswa na maisha na afya ya Mtanzania mwenzake hasa linapokuja suala la kusaidia kupata damu salama ili kunusuru uhai.

Maadhimisho hayo siku zote yamekuwa yakisisitiza katika kila mmoja kuona kuwa ana jukumu la kuchangia ama kusaidia wagonjwa wanaohitaji msaada wa kuongezewa damu kwani kufanya hivyo ni kuguswa na kuishi ukweli kuwa damu ni uhai na ndiyo maisha na bila damu maisha yanakuwa kwenye hatihati.

Siku hiyo pia inaangazia umuhimu wa kutoa damu mara kwa mara ili kuwezesha kupata akiba lakini pia kumudu kusambaza damu salama na endelevu katika hospitali mbalimbali nchini kulingana na mahitaji hayo maalumu kwa maisha ya kila binadamu.

Leo ni Juni 14 ndiyo maadhimisho ya siku hii maalumu ya kuchangia damu na mkoa wa Dar es Salaam, umeeleza nia yake ya kufanya kampeni maalumu ya vituo vyote vinavyofanya kazi hiyo maalum ya kukusanya damu.

Watanzania mmoja mmoja, taasisi na jumuiya mbalimbali ni vyema kuichukulia Juni 14 kuwa siku yetu au ya kila mtu, kwa kuhamasishana na kutoa damu ili iwe siku muhimu na Watanzania wajitokeze kwa wingi katika kufanikisha zoezi hilo.

Kampeni kwenda vizuri ni kupatikana kwa damu kwa wingi kwa maslahi ya wagonjwa na wahitaji popote walipo kwenye vituo vya huduma za afya.

Ni vyema kukumbuka kuwa suala hilo si la mtu binafsi bali ni la Watanzania wote wake kwa waume hivyo ni shime wajitokeze katika vituo kufanikisha zoezi hilo.

Kwa wakazi wa mkoa wa Dar es Salaam ni vyema kujitokeza kwa wingi kuiunga mkono kampeni hiyo ya kufanikisha jukumu la kukusanya damu ambalo ni jambo la heri duniani na pia lina malipo kwa Mwenyezi Mungu.

Awali Machi 20 hadi 24 mwaka huu, Wizara ya Afya chini ya Mpango wa Taifa wa Damu Salama uliopo kwenye Ofisi ya Rais TAMISEMI iliendesha kampeni maalumu ya ukusanyaji wa damu ili kuimarisha benki ya damu nchini.

Lengo la kampeni hiyo ilikuwa ni kukusanya chupa za damu 22,000 kwa mikoa yote 26 na matokeo chanya ya zoezi hilo yalipatikana na kupatikana kwa jumla ya chupa 18,334 sawa na asilimia 83.

Hayo ni malengo ya kudumu katika kutetea uhai na ukweli ni kwamba zoezi limefanyika lakini bado kumekuwa na upungufu wa asilimia 17 kutimiza malengo ya kufikia chupa 22,000.

Mpango wa damu salama mara kwa mara umekuwa ukifanya kampeni mbalimbali kukusanya damu kuwezesha mfuko huo kukua na hatimaye benki ya damu kuwa na akiba ya kutosha kuhudumia wagonjwa wenye uhitaji huo bila kutetereka.

Vituo vya uchangiaji damu hiyo ikiwamo Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete, hospitali za Amana, Temeke, Mwananyamala, Mbagala Rangi tatu, Mnazi Mmoja, Sinza, eneo wafanyabishara wamachinga Karume, Feri na manispaa ya Kigamboni, vimejibidiisha kutimiza lengo hilo.

Aidha, ni wito kuwa shime watu wajitokeze leo kuchangia damu kuokoa maisha ya wahitaji, ikumbukwe kuwa kila mtu ni mgonjwa mtarajiwa kadhalika mhitaji damu mtarajiwa pia.

Kuna ajali, yapo maradhi kama malaria kwa wazima, wajawazito na watoto ambayo huleta matatizo ya upungufu wa damu hivyo ukiwa mzima kumbuka kuwa kuna wahitaji.

# Maofisa ugani waipa kongole AMDT kuelimisha wakulima

**Na Maulid Mmbaga,** TABORA

MAOFISA ugani mkoani Tabora wameipongeza Taasisi ya Kuboresha Mifumo ya Masoko ya Kilimo nchini (AMDT) kwa kuwapatia elimu ya kilimo bora ili kuongeza tija katika uzalishaji wa alizeti na jamii ya mikunde.

AMDT imewekeza Sh. bilioni nne kwa ajili ya kuwawezesha wakulima, ikishirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) kuratibu mradi unaohamasisha matumizi ya mbegu bora ya alizeti na jamii ya mikunde kwa lengo la kuongeza uzalishaji na tija katika sekta ya kilimo.

Akizungumza na waandishi wa habari waliotembelea shamba lililoko Kijiji cha Kapumpa, Wilaya ya Sikonge mkoani Tabora jana, Bwanashamba kutoka Kampuni ya Lima Africa, Roance Rwegasila alisema zaidi ya wakulima 250 katika mkoa huo wameendelea kunufaika na mradi huo baada ya kufanikiwa kuzalisha zaidi ya tani 25 za mbegu bora za alizeti katika msimu wa kwanza wa ushirikiano baina yao, AMDT na TARI.

Alisema wamefanikiwa kulima ekari 70 za alizeti na vikundi vya wakulima vya wanawake na vijana ambao ni miongoni mwa wakulima hao 250.

"Mradi umefanikiwa kutoa elimu, ajira na pembejeo kwa wakulima hao ambao 150 ni wanawake na 100 ni vijana kupitia kampuni ya uzalishaji mbegu ya Lima Africa, ambayo ni moja ya washirika wa AMDT na TARI, ambayo imekuwa ikitusimamia ili kuhakikisha tunatoka kwenye kilimo cha mazoea na kufanya kilimo biashara ambacho kimesaidia kubadilisha uchumi wa wakulima wengi," alisema Rwegasila.

Aliongeza kuwa wanaendelea kutoa mafunzo na elimu ya shamba darasa kwa zaidi ya wakulima wengine 150, namna ya kulima, ikiwa kuna upungufu wa mvua, jinsi ya kukabiliana na wadudu na kufuata taratibu zote za kisasa.

Akielezea mafanikio ya mradi huo Katibu wa Kikundi cha kinamama cha Nguvu Kazi, Leah Robert, alisema kikundi chao kilikuwa kinalima kienyeji na kilikuwa kinapata mavuno yasiyoridhisha, hivyo kuwakatisha tamaa.

"Baada ya kupata elimu ya kilimo bora chini ya AMDT, Lima na TARI, sasa tunapata magunia kuanzia matano na kuendelea, kitu ambacho ni tofauti na zamani tulikuwa tunapata gunia moja au mawili kwa ekari," alisema Leah.

Msimamizi wa shamba hilo lililoko nje kidogo ya Wilaya ya Sikonge, Paul Daniel, alisema licha ya changamoto za kimazingira bado mwitikio ni mkubwa kwa vijana na wanawake na unaongezeka siku hadi siku.

"Hapo mwanzo baada ya mradi kuanza wengine walikuwa wanatubeza, lakini siku zilivyokuwa zinakwenda na wao wakavutiwa na kujiunga na sisi ili kuanza kuzalisha na wakaanza kuchukulia kama fursa," alisema Daniel.

# Mshtakiwa kesi ya kulawiti agoma kujitetea dakika nane

**Na Grace Gurisha**

MSHTAKIWA anayetuhumiwa kumlawiti mtoto wa miaka 12, Juma Rashid ametumia dakika nane kukataa kujitetea mbele ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Kinondoni kwa madai kuwa hana cha kujitetea, hivyo mahakama itoe uamuzi.

Mahakama hiyo ilimuuliza zaidi ya mara nane kama anauhakika na kile alichokitaka kwa kuwa sheria inaelekeza kitakachochukuliwa na mahakama ni kile kilichotolewa na upande wa mashtaka, lakini mshtakiwa aliendelea kubaki na msimamo wake huo.

Rashid alitoa msimamo huo juzi mbele ya Hakimu Mkazi Aron Lyamuya wa mahakama hiyo, baada ya kuelezwa kwamba anatakiwa kujitetea kutokana na ushahidi wa mashahidi wanne na vielelezo vilivyotolewa mahakamani dhidi yake.

"Mshtakiwa unatakiwa uieleze mahakama utajitetea kwa kiapo, bila kiapo au kukaa kimya mahakama ndiyo iamue," alisema Hakimu Lyamuya

Mshtakiwa: Ninaichia mahakama itoe uamuzi

Hakimu: Unajua unachokijibu wewe? Sheria inaeleza kwamba kitachukuliwa kilekile ambacho kimetolewa mahakamani hapa.

Mshtakiwa: Sina cha kujitetea wewe toa uamuzi

Hakimu: Kwa hiyo, ninaweza kusema kuwa una hatia?

Mshtakiwa: Mimi sina cha kujitetea, nitajitetea nini sasa?

Hakimu: Una hakika na chaguo lako ulilolichagua? Haya mpeni hii karatasi atie saini alichokichagua.

Mshtakiwa akapatiwa karatasi na karani iliyotolewa na Hakimu Lyamuya ili aitie saini. Aliichukua na akataka kutia saini.

Hakimu: Ninakuuliza kwa mara nyingine, una uhakika na unachotaka kukitia saini?

Mshtakiwa: Mimi sina cha kujitetea.

Hakimu: Haya, tia saini.

Mshtakiwa: Basi sisaini tena.

Hakimu: Unakunywa sumu halafu unajaribu kama itakuua au la?

Mshtakiwa akacheka, hakimu akamuuliza

"kwa hiyo utajitetea kwa njia gani? Akajibu 'bila kiapo'.

Mshtakiwa Rashid alikubali kujitetea kwa njia ya kiapo, akitumia muda mrefu kukubaliana na hilo.

Awali, Wakili wa Serikali, Daisy Makakala, akimwongoza shahidi namba nne ambaye ni Daktari wa Kituo cha Afya Kawe, Jesca Bunyaga (59), alidai kuwa katika uchunguzi wake alibaini kuwa mtoto huyo (jina limehifadhiwa) alikuwa ameingiliwa sehemu za siri za nyuma.

"Mtoto huyu alikuwa na umri wa miaka 12 na kwa jinsi nilivyoona na ishara nilizoziona, niligundua kwamba si mara yake ya kwanza kuingiliwa. Ingekuwa ni mara ya kwanza ningeona michubuko," alidai Dk. Bunyaga.


## NOTISI / TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,YARDLEY RECOVERIES AUCTION LTD, SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya Benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC**, tunatoa notisi ya kurudia minada ya hadhara kama ilivyohainishwa kwenye tangazo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| HEAD OFFICE | PROJEST ELISANT MASSAWE | PAGALE LA NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA.24,KITALU '12' HATI NAMBA 145148 | PROJEST ELISANTEMASSAWE | MABWEPANDE -KINONDONI | 28/06/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | DIANA CLIFFORD KURUCHUMILA | NYUMBA | DIANA KURUCHUMILA | MBEZI MSAKUZI | 28/06/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | FELIX SIMON MAVUMBO | NYUMBA | ZAWADI FABIAN KAHOHO | VIANZI- MKURANGA | 05/07/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | ABDALLAH AHMAD MUHIDINI | NYUMBA | ABDALLAH AHMAD MUHIDINI | TEGETA A - GOBA | 29/06/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | MWANAHAMISI MSOFE BEDA | NYUMBA | MWANAHAMISI MSOFE BEDA | KIYOMBO- KITUNDA | 30/06/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | MELANIA RAYMOND KILEWO | NYUMBA | MELANIA RAYMOND KILEWO | MIPEKO-TAMBANI MKURANGA | 05/07/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | KENETHI HEZRONI CHIBANILA | NYUMBA | KENETHI HEZRONI CHIBANILA | MJI MPYA-VEYULA | 28/06/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | VERONICA AGOSTINO SHANA | PAGALE LA NYUMBA | VERONICA AGOSTINO SHANA | NZUGUNI 'A' | 30/06/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | IMAN SAJENI SANGA | PAGALE LA NYUMBA | IMAN SAJENI SANGA | CHIMALAA NTYUKA | 29/06/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | BAHARI BAKERY LIMITED | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA.339,KITALU 'E' HATI NAMBA 51256 | STEPHANO VICENT | KUNDUCHI -TEGETA | 28/06/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| HEAD OFFICE | ALIPO BERNARD CHIKOKO | KIWANJA | ALIPO BERNARD CHIKOKO | BOKOTIMIZA-KIBAHA | 19/07/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| HEAD OFFICE | CELESTINE MSIMBU SHIJA | KIWANJA | CELESTINE MSIMBU SHIJA | BOKOTIMIZA-KIBAHA | 19/07/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja, au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.

2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.

3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.0759282344/0765999000/0754497396/0715868000

4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

# Waziri atangaza mazao utalii yanayopatikana Tanzania pekee

**Na John Mapepele**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Mohamed Mchengerwa, ametangaza mazao rasmi matatu ya utalii ambayo hayapatikani nchi yoyote duniani isipokuwa Tanzania, akiwaomba Watanzania kuyatumia na kuyatangaza ili wageni kutoka sehemu mbalimbali kuja kuona.

Mchengerwa alitangaza mazao hayo jana alipokuwa na Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Hassan Abbasi, pamoja na Menejimenti ya Bodi ya Utalii nchini kumtangaza Mwanamitandao ya kijamii maarufu nchini na duniani, Nicholas Reynolds, maarufu Bongozozo, ambaye ana mtandao mpana unaojumuisha blogu mbalimbali za kimataifa zinazowafikia watu zaidi ya milioni 100 duniani.

Waziri Mchengerwa aliyataja mazao hayo matatu ya utalii ambayo hayapatikani sehemu yoyote duniani isipokuwa Tanzania kuwa ni; tukio la msafara wa wanyama nyumbu katika Hifadhi ya Taifa Serengeti, maarufu Great Migration, tukio la kutembea kwa miguu kwa wageni katikati ya Hifadhi ya Taifa Ruaha umbali wa takriban Km 50 na kuwapo msafara wa makundi makubwa na kuweka makazi kwa samaki mkubwa kuliko wote duniani Potwe, maarufu Papa Usingizi katika Hifadhi ya Bahari ya Kisiwa cha Mafia.

Alifafanua kuwa mazao yote hayo matatu hayapatikani mahali popote duniani isipokuwa Tanzania. Pamoja na kuwapo kwake, watu wengi hawayatambui kwa kuwa hayajatangazwa kikamilifu, hivyo kutoa wito kwa Bodi ya Utalii nchini kutokana na kutangaza mazao hayo kikamilifu.

"Ndugu zangu ni vizuri kutambua kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi chache duniani na ya kwanza Afrika kwa kuwa na vivutio vingi vya utalii lakini havijatangazwa, hivyo nitoe wito kwa Watanzania wote kuwa wazalendo na mabalozi wa kutangaza na kuthamini urithi huu tulipewa na Mwenyezi Mungu," alisisitiza.

Alimwomba Bongozozo kuwa balozi mzalendo na bora wa Tanzania ili kutumia umaarufu na mtandao wake kuutangaza utalii wa Tanzania kila kona ya dunia huku akiitaka Bodi ya Utalii nchini kupitia orodha ya mabalozi wa heshima kuona wale wasiofanya kazi na kuwaondoa ili kubaki na wachapakazi.

Bongozozo, raia wa Uingereza ambaye ameoa na kuishi Tanzania kwa muda mrefu, aliahidi mbele ya Waziri Mchengerwa na Katibu Mkuu, Dk. Abbasi, kuwa atatumia ipasavyo ushawishi wake duniani kuutangaza utalii wa Tanzania.

Mkurugenzi wa Masoko wa Bodi ya Utalii nchini, Dk. Glladstone Mlay, alisema kuwa kwa sasa Bongozozo anaanza ziara yake kutangaza vivutio vya utalii kusini mwa Tanzania ikiwa ni utekelezaji wa mkakati wa utangazaji utalii kusini mwa Tanzania wa 2021-2026 ambao uliandaliwa kupitia mradi wa REGROW na kuzinduliwa Septemba 2022 mkoani Njombe.

Alisema mkakati huo umetaja njia mbalimbali za utangazaji utalii wa kusini mwa Tanzania ikiwa ni pamoja na kutumia watu maarufu/mabalozi wa hiari, utangazaji kwa njia ya mtandao, vyombo vya habari, safari za mafunzo na kushiriki katika maonyesho ya kibiashara na matukio.

Waziri Mchengerwa aliwakaribisha Watanzania wote kujumuika na Bongozozo katika kutembelea vivutio vya utalii vya nyanda za juu kusini ambavyo kwa sasa serikali imeongeza nguvu kupitia mradi wa Usimamizi Rasilimali za Maliasili kwa Utalii na Endelevu (REGROW) na kuendelea kuunga mkono jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan kutangaza Tanzania kupitia filamu ya Tanzania The Royal Tour.




Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano wa Benki ya Exim, Stanley Kafu (kushoto), akichangia damu sambamba na wadau wengine waliojitokeza wakati wa zoezi la uchangiaji damu lililoandaliwa na benki hiyo jijini Dar es Salaam jana, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Uchangiaji Damu Duniani. Anayewahudumia ni Ofisa wa Mpango wa Taifa wa damu salama (NBTS), Salma Ramadhani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafanyakazi, wateja Benki ya Exim wachangia damu

**Na Mwandishi Wetu**

WAFANYAKAZI wa Benki ya Exim Tanzania, wateja na wadau wengine katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya, Dodoma na Mtwara jana walijitokeza kwa katika matawi ya benki hiyo na maeneo maalum yaliyoandaliwa na benki hiyo ili kuchangia damu ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha Siku ya Uchangiaji Damu Duniani.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati uchangiaji ukiendelea, Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano wa Benki ya Exim, Stanley Kafu, alisema hatua hiyo ni mwendelezo kwa kuwa wamekuwa wakifanya hivyo tangu mwaka 2010 na lengo ni kukabiliana na tatizo la uhaba wa damu salama katika vituo vya afya nchini.

"Mara zote tumekuwa tukijisikia kuwa na wajibu mkubwa kama benki ya kizalendo kila tunapoelekea maadhimisho muhimu haya ya uchangiaji damu kwa kuwa tunaamini kwamba tunapata fursa ya kutimiza wajibu wetu kama sehemu ya jamii lakini pia kwa kufanya hivyo tunakuwa tumeshiriki kuokoa maisha ya wenzetu wakiwamo kinamama, watoto na waathirika wa ajali wanaopoteza maisha kwa kukosa damu salama pale wanapoihitaji," alisema.

Ni hoja inayokwenda sambamba na kaulimbiu ya uchangiaji damu ya mwaka huu inayosema: 'Changia Damu, Changia Mazao ya Damu (Plasma), Changia mara kwa mara', inayolenga kuonyesha namna gani maisha ya watu wenye uhitaji wa damu huokolewa na wenzao wanaojitokeza kuchangia damu mara kwa mara.

"Kufuatia mafanikio makubwa na uungwaji mkono tunaoupata kupitia kampeni hii, Benki ya Exim tunawashukuru sana wafanyakazi wa benki kwa namna wanavyojitolea kuchangia damu kila linapofanyika zoezi hili. Shukrani hizi pia tunazielekeza kwa wateja wetu na wadau wengine ambao waliojumuika nasi leo katika mikoa mitano tunayoendesha zoezi hili.

"Ushirikiano huu baina yetu na wadau wetu unathibitisha uhusiano imara kati ya benki na jamii tunayoihudumia ambao kimsingi unakwenda nje ya mipaka ya biashara hadi kwenye hatima ya maisha yetu," alisema.

Akizungumza wakati akisimamia uchangiaji damu, Ofisa Uhamasishaji na Elimu kwa Umma kutoka Mpango wa Taifa wa Damu Salama (NBTS), Marry Meshy, alisema uhaba wa damu nchini umekuwa ukichangiwa kwa kiasi kikubwa na mtazamo wa wananchi walio wengi kwamba wapo tayari kuchangia damu pale tu inapohitajiwa na mmoja wa ndugu wa familia husika.

"Hivyo basi, ninatoa wito kwa wananchi mmoja mmoja pamoja na taasisi nyingine kuiga mfano wa Benki ya Exim Tanzania ambayo imekuwa na utamaduni wa kuchangia damu kila mwaka ili kuokoa maisha ya Watanzania wote," alisema.

Alibainisha kuwa kupitia maadhimisho hayo, NBTS Kanda ya Mashariki wanategemea kukusanya chupa za damu 1,500, malengo ambayo yamefanikiwa kwa asilimia 60 hadi kufikia jana.

# SBL kupanua wigo ununuzi malighafi wakulima wadogo

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti, mmoja wa wazalishaji wakubwa wa bia nchini, amesema inalenga kuongeza vyanzo vyake vya malighafi kutoka kwa wakulima wadogo hadi kufikia asilimia 85 ya jumla ya malighafi zake katika mwaka ujao wa fedha.

Kwa sasa kampuni hiyo inapata asilimia 70 ya malighafi zake kutoka kwa wakulima wa ndani ambao wako chini ya mpango wa kilimo cha mkataba na kampuni ya bia.

SBL ilianza kushirikisha wakulima katika mfumo wa kilimo cha mkataba miaka 10 iliyopita, yaani mwaka 2013. Wakulima hutoa malighafi kama vile mahindi, shayiri na mtama kwa kampuni hiyo ya bia.

Kampuni hiyo inawavutia wakulima wa ndani kushiriki katika mpango huo kama njia ya kuwawezesha kwa kuwapatia mafunzo ya kilimo na vifaa vya kilimo kama mbegu na mbolea, pia kuwawezesha kupata huduma za bima ya mikopo. Kwa sasa, SBL inashirikiana na wakulima wadogo katika mikoa saba, ambayo ni Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Mwanza, Mara, Singida na Shinyanga.

Meneja wa Mawasiliano na Uendelevu wa SBL, Rispa Hatibu, alisema jana kuwa "...chanzo kikuu cha malighafi yetu kwa ajili ya uzalishaji kinatokana na mazao ya kilimo.

"Hivyo tumekuwa tunafanya kazi kwa karibu katika ushirikiano na wakulima wetu wadogo wa ndani ili kupata malighafi kutoka kwao. Kupitia mkataba huu, tunashirikisha wataalamu wetu wa kilimo kuwajengea wakulima wetu wadogo ujuzi wa kilimo na kuwapatia pembejeo muhimu za kilimo ili wazalishe nafaka za kutosha ambazo zina viwango vinavyotakiwa.

"Hatimaye, wakulima wana uwezo wa kuzalisha mavuno ya kutosha ambayo wana masoko tayari. Kimsingi tunachukulia mpangilio huu kama ushirikiano wa kushinda-kushinda."

Msaada wa SBL unategemea kuwezesha mafunzo kwa wakulima wadogo wanaofanya kazi na kampuni hiyo ya bia, kununua pembejeo za kilimo na kuwezesha mipango ambayo itawawezesha wakulima wadogo kufanya kilimo kwa njia endelevu zaidi.

Kutokana na mafanikio kama hayo, ambayo yanawanufaisha SBL na wakulima wadogo, ofisa huyo SBL itaendelea kuwekeza katika maendeleo ya wakulima wadogo kwa kuwezesha kufanya kilimo endelevu na kuboresha sekta ya kilimo kwa ujumla.

"Nia yetu ya kuongeza idadi ya wakulima wanaoshirikiana nao na hata kufikia mikoa zaidi, inakwenda sambamba na juhudi zetu za kuchangia katika sekta ambayo ni uti wa mgongo wa uchumi wa nchi yetu," alisema.

Zaidi ya wakulima wadogo 400 katika mikoa saba ambayo SBL inashirikiana na wakulima, wamekuwa wakinufaika na mpango wa kilimo cha mkataba wa kampuni hiyo ya bia.

Hatibu alisema SBL pia imekuwa ikitekeleza kwa mkakati programu ya udhamini kwa wanafunzi kutoka kaya maskini ambao wanaochukua masomo ya kilimo katika vyuo kwa lengo la kuwajengea ujuzi sahihi wa kilimo. Programu hiyo inayojulikana kama Kilimo Viwanda ina manufaa kwa wanafunzi kutoka familia za wakulima. Kupitia programu ya udhamini, SBL inahusika na gharama zote za masomo kwa wahusika.



## EWURA yawaonya wananchi wanaowatumia vishoka

**Na Allan Isack,** BABATI

MAMLAKA ya Uthibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imetoa onyo kwa wananchi wanaowatumia vishoka kuwafungia mifumo ya umeme, kwamba itawachukulia hatua kali za kisheria.

Onyo hilo lilitolewa jana Mjini Babati na Meneja wa EWURA Kanda ya Kaskazini, Lorivii Long'idu, wakati akitoa mafunzo kwa wanafunzi wanaosoma fani ya ufundi mchundo kwa vyuo vya ufundi stadi yaliyohusu umuhimu wa kuwa na leseni, kupunguza vishoka.

"Serikali kupitia mamlaka hiyo, imeanza kutekeleza mpango unaolenga kudhibiti vishoka wanaounganisha mifumo ya umeme kwenye maeneo ya makazi na taasisi.

"Sasa kutokana na baadhi ya wananchi kuwatumia vishoka, imekuwa chanzo cha kusababisha majanga ya hitilafu za umeme kwenye maeneo mbalimbali ikiwamo kwenye makazi, viwanda na taasisi," alisema.

Alisema ili kudhibiti suala hilo wameanza kutoa mafunzo ya umuhimu wa mafundi mchundo kuwa na leseni za umeme huku akiwaonya wananchi wanaoendelea kutumia mafundi umeme wasiokuwa na leseni zinazotolewa na EWURA kuacha tabia hiyo.

"Lengo la kutoa elimu ya uombaji wa leseni ni kuhakikisha kazi za umeme zinafanywa na watu ambao ni wataalamu waliosoma kwa kuwa hao ndiyo wanaweza kufanya kazi kwa kuzingatia viwango na ubora wa kazi hali itakayosaidia kupunguza maafa yanayoweza kutokea kutokana na majanga ya moto yatakayosababisha watu kupoteza uhai na mali," alisema Long'idu.

Aidha, alisema lengo lingine ni kuhakikisha wanathibiti majanga ya moto ambayo yanaweza kusababishwa na moto wa umeme kutokana na kazi zinazofanywa chini ya kiwango ambazo zilitakiwa kufanywa na wataalamu wanaotambulika na serikali.

Mhandisi Mwandamizi wa Umeme kutoka EWURA Kanda ya Kaskazini, Tegemea Kamando, aliwataka wanafunzi hao kuwa mabalozi kwa mafundi wengine, waache tabia ya kutegemea leseni ya mwingine ili kupata kazi.

# Serikali yatoa bil. 15/- kukamilisha miradi ya elimu, afya Kilimanjaro

**Na Mary Mosha,** SIHA

ZAIDI ya Sh. bilioni 15 zimetolewa katika mwaka wa fedha 2022/2023 kwa ajili ya kukamilisha miradi ya elimu, afya, miundombinu ya barabara ili kuwawezesha wananchi wa Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro kufikia mahitaji mbalimbali ikiwamo kuinua kipato.

Mkuu wa Wilaya ya Siha, Dk. Christopher Timbuka, alieleza hayo jana wakati Kamati ya Siasa ya Mkoa wa Kilimanjaro ilipotembelea na kukagua miradi mbalimbali ikiwamo ile inayotekelezwa kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Kamati hiyo ya siasa inaongozwa na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama Cha Mapinduzi (NEC), Suleman Mfinanga. Kamati hiyo ilikagua miradi katika vijiji cha Kyengia, Munge, Mkombozi, Naibili Sanya Juu na Wiri.

"Tumeona na kukagua vyumba vitano vya madarasa katika Shule ya Msingi Kyengia, ujenzi wa Shule ya Msingi Munge, tumekagua Kituo cha Afya Olkolili, vyumba vinne vya madarasa na matundu ya vyoo 28 katika Shule ya Sekondari Biriri.

"Vilevile, tumekagua Hospitali ya Wilaya ya Siha, ambayo walipata fedha kwa ajili ya upanuzi na barabara ya Mkuu wa Wilaya/Magadini. Hakika thamani ya fedha inaonekana, ingawa tumeshauri kuendeleza kasi ya utendaji kutokana na kuwepo kwa fedha," alisema Mfinanga.

Awali, Mkuu wa Wilaya hiyo, Christopher Timbuka, alisema siri kubwa ya kukamilika miradi hiyo kwa asilimia 89 ni usirikishwaji wa wananchi.

Alisema pamoja na Sh. bilioni 15, pia kati ya Mei na Juni mwaka huu, wamepokea tena zaidi Sh. milioni 999 ya mradi wa Kuimarisha Ufundishaji na Ujifunzaji kwa Shule za Awali na Msingi Tanzania (BOOST), kwa ajili ya kujenga na kukarabati shule uchakavu.

Imo pia, Sh. bilioni 2. 32 zilizotolewa kwa ajili ya ujenzi wa mabweni, vyoo na madarasa, kwa ajili ya shule za sekondari za kidato cha tano na sita.

Alisema: "Asilimia 95 ya miradi inayoendelea wilayani hapa, zinatarajiwa kukamilika Juni 30, mwaka huu. Tumepokea ushauri wa marekebisho madogo madogo, ikiwamo ya namna bora ya kumalizia, kusubiri mbao kukauka na kuongeza kasi ya utendaji ambavyo vyote tutavisimamia".




Meneja wa Air France–KLM Tanzania, Alexander van de Wint (kushoto), Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Fatma Mohamed Rajab (wa pili kushoto), Makamu wa Rais wa Air France–KLM Afrika, Jean-Marc Pouchol (wa pili kulia) na Meneja Mkuu wa Air France-KLM kwa Afrika Mashariki na Kusini, Nigeria, na Ghana, Marius van der Ham, wakikata keki kusherehekea uzinduzi wa safari ya kwanza ya Air France kutoka Paris Charles de Gaulle hadi Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam juzi, itakayoendeshwa mara tatu kwa wiki Jumatatu, Jumatano na Jumamosi na Boeing 787-9. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Usimamizi hafifu chanzo huduma mbovu vituo vya afya

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki, amesema usimamizi hafifu wa vituo vya afya nchini husababisha vituo hivyo kutoa huduma zisizoridhisha.

Amesema pia kutotumia fedha kwa wakati zinazotokana na mapato ya uchangiaji wa huduma za afya, Mfuko wa Afya wa Pamoja na Global Fund, kunasababisha vituo kuwa na bakaa kubwa.

Aliyasema hayo jana jijini Arusha wakati akifungua kikao kazi cha siku mbili cha waganga wakuu na waratibu wa UKIMWI wa halmashauri nchini, kilichoenda sambamba na uzinduzi wa Mfumo wa Kielekroniki wa Usimamizi wa Taarifa za Mfumo wa Mshitiri (PVMIS).

Kairuki alisema katika kipindi cha kuanzia Januari, 2021 hadi Januari 2023 kupitia Mfuko wa Global Fund, Sh.bilioni 32.2 zilitumwa katika Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali, ikiwamo uboreshaji wa miundombinu.

Alisema hadi kufikia Januari, 2023 Sh. bilioni 4.9 bado hazijatumika hali inayosababisha nchi kukosa fedha zingine za ujenzi wa miundombinu husika.

Vile vile, alitumia fursa hiyo kuwaagiza wakurugenzi wa halmashauri, waganga wakuu wa mikoa na halmashauri, waganga wafawidhi wa vituo kuongeza uwajibikaji na kusimamia vituo hivyo ipasavyo na kuhakikisha fedha zote zilizopo vituoni zinatumika kwa wakati na kuzingatia mipango.

Alisema Ofisi ya Rais TAMISEMI imeendelea kusimamia huduma za ustawi wa jamii katika la eneo la familia, malezi, makuzi, maendeleo ya awali ya mtoto, huduma kwa wazee na watu wenye ulemavu.

Alisema hadi kufikia Februari mwaka 2023 watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi 335,971 walitambuliwa, kati yao 26,000 sawa na asilimia 7.7 walipewa huduma mbalimbali kama chakula, malazi, mavazi na matibabu. Vilevile, alisema mashauri 13,926 ya ukatili wa kijinsia yalilipotiwa, kati ya hayo 7,142 sawa na asilimia 56 yalikuwa ni dhidi ya wanawake na 6,784 sawa na asilimia 51 yalikuwa dhidi ya watoto, mashauri 1,199 yalifikishwa mahakamani, kati ya hayo 430 sawa na asilimia 36 yalitolewa hukumu.

"Naendelea kuwasisitiza waganga wakuu wa halmashauri, moja kuhuisha kamati za ulinzi kwa wanawake na watoto, katika ngazi zote, mbili kuhakikisha mashauri ya kesi za watoto, ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto, unasimamiwa ipasavyo mahakamani, huku wakiendelea kuwatambua watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi na kuwanganisha na huduma stahiki," alisema.


Kadhalika alisema, jukumu kubwa la TAMISEMI ni kuendelea kusimamia afua za lishe ikiwa ni pamoja na kupeleka huduma za lishe katika ngazi ya wananchi.

Alisema ili kufikia dhima hiyo ni lazima viongozi ngazi ya mikoa na halmashauri kuhakikisha wanatekeleza haraka zaidi afua za lishe katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya.

Kadhalika, aliziagiza halmashauri ziendelee kutenga Sh.1,000 kwa kila mtoto mwenye umri chini ya miaka mitano katika maeneo yao na kuhakikisha kuwa usimamizi unafanyika, ili zitumike kutekeleza afua za lishe zenye kuleta matokeo chanya na ya haraka. Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), anayeshughulikia masuala ya afya, ustawi wa jamii na lishe, Dk. Charles Mahera alisema kikao hicho kina lengo la kujengeana uwezo ili kutoa huduma bora za afya katika vituo vya afya msingi vilivypo nchini.

Alisema serikali imetenga zaidi ya Sh. bilioni 950 kwa ajili ya huduma za afya ikiwamo ujenzi wa hospitali, zahanati na vituo vya afya na Sh.bilioni 200 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba ili kuboresha huduma za afya nchini.

Mkurugenzi wa Huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe katika Ofisi ya Rais TAMISEMI, Dk. Ntuli Kapologwe, aliipongeza Serikali ya Uswisi kwa ufadhili wa uundwaji wa mfumo huo kupitia mradi wa HPSS Tuimarishe Afya.





# RC atoa siku saba wakulima tumbaku kulipwa bilioni 20/-

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Batilda Burian, ametoa siku saba kwa kampuni ya ununuzi wa tumbaku mkoani humo ya Voedsel kuhakikisha inawalipa wakulima wa zao hilo deni la Sh. bilioni 20.

Amesema endapo watashindwa kutekeleza agizo hilo ameahidi kuwaweka ndani.

Alitoa kauli hiyo juzi alipokutana na viongozi wa kampuni hiyo ofisini kwake baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wakulima juu ya ucheleweshaji wa malipo yao pindi wanapowauzia tumbaku.

Balozi Dk. Batilda alisema kwamba serikali haitavumilia tabia ya ucheleweshaji wa malipo kwa wakulima jambo ambalo linaendelea kurudisha nyuma uzalishaji wa zao hilo pamoja na maendeleo ya wakulima kwa ujumla.

Alisisitiza kuwa maelekezo ya serikali katika msimu huu wa masoko ni lazima kila mkulima alipwe fedha zake ndani ya saa 48 baada ya soko, lakini kampuni hiyo imekaa na pesa za wakulima hao kwa zaidi ya siku 40 kinyume na makubaliano.

"Sisi hatulichukulii hili kama deni bali ni wizi wa kuaminika maana Rais Samia Suluhu Hassan alitaka wakulima walipwe ndani ya siku mbili na vyama vingine vimelipa, hatuwezi kuwaruhusu kuendelea kununua mpaka mmemaliza madeni haya yote," Dk. Batilda.

Hata hivyo Meneja wa Kanda wa Bodi ya Tumbaku Kanda ya Magharibi, Albert Charles, alisema bodi hiyo imeiondoa kwenye ratiba ya masoko kampuni hiyo mpaka itakapokamilisha ulipaji wa madeni ya wakulima.

Meneja wa kampuni ya Voedsel Mkoa wa Tabora, Victor Matawa, alimweleza mkuu huyo wa mkoa kuwa wataanza kulipa madeni yote ya wakulima kabla ya kumalizika kwa wiki ijayo ili kuhakikisha kila mkulima anapata haki yake.

Alisema kuwa mchakato na utaratibu wa kuwalipa wakulima utaanza mara moja baada ya kukamilisha tatizo la kifedha ambalo lilikuwa likitatuliwa na Benki ya CRDB.

Kampuni hiyo mpaka sasa imelipa Dola za Marekani milioni moja kati ya Dola za Marekani milioni nane wanayodaiwa na vyama vya ushirika vya WETCU na Milambo Union.

Wakizungumza na Nipashe hivi karibuni wanachama hao walieleza kuwa kampuni hiyo ina masoko matatu ambapo soko la kwanza lilifanyika 27 Aprili 2023, chama kilikuwa na jumla ya kilo 1,408,748.



Wakulima wa mbegu ya alizeti wa kikundi cha Chapakazi Kijiji cha Kapompa, Wilaya ya Sikonge mkoani Tabora, wakichambua uchafu kwenye mbegu bora aina ya record ambayo wamelima baada ya kupata elimu kutoka Taasisi ya Kuboresha Mifumo ya Masoko ya Kilimo nchini (AMDT). **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## Zahanati yapandishwa hadhi kuondoa adha wananchi

**Na Marco Maduhu,** KAHAMA

WANANCHI wa Bugarama Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wameondokana na adha ya kufuata huduma za matibabu umbali mrefu baada ya Zahanati ya Bugarama kuboreshwa na kuwa kituo cha afya.

Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Bugarama, Dk. Silas Kayanda, alisema awali wananchi wa Bugarama na vijiji jirani walikuwa wakipata shida kupata huduma bora za afya karibu, kulazimika kufuata huduma hizo wilayani Kahama zaidi ya kilomita 73.

"Mgodi wa Barrick Bulyanhulu uliboresha miundombinu pamoja na kuwezesha vifaa tiba vya kisasa, hali iliyofanya zahanati hii kupandishwa ambako kwa sasa huduma zote bora za matibabu zinapatikana hapa hakuna tena kwenda Kahama,"alisema Dk. Kayanda.

Alisema kutokana na kituo hicho kuwa na vifaa tiba vya kisasa wamekuwa wakipokea wagonjwa wengi tofauti na hapo awali, ikiwa ni pamoja na mama wajawazito wakifungulisha wajawazito 180 hadi 250 kwa mwezi.

Mmoja wa wagonjwa anayepatiwa matibabu katika kituo hicho cha afya, Robert Nkwambi, alisema awali walikuwa wakiteseka kupata huduma bora za matibabu lakini sasa hivi huduma zote wanazipata hapo hali inayowasaidia kutekeleza majukumu yao kwa wakati.

Kaimu Meneja Mahusiano ya Jamii kutoka Mgodi wa Barrick, Bulyanhulu Zuwena Senkondo, alisema mgodi huo umekuwa ukiwathamini wananchi wanaozunguka na kuwapatia huduma mbalimbali kupitia fedha za huduma za jamii na kuwatekelezea miradi ya maendeleo ikiwa ni pamoja na hiyo ya sekta ya afya.

Alisema katika Kituo cha Afya Bugarama wanatarajia kujenga jengo la mionzi ili kiendelee kutoa huduma bora za matibabu kwa wananchi na kwa wakati.

# Vijana 650 wajitokeza kufanyiwa tohara

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

VIJANA zaidi ya 650 wamejitokeza kupata huduma ya tohara katika Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, katika kipindi cha Oktoba 2022 hadi Juni mwaka huu.

Hali hiyo ni ongezeko kubwa kutokea kutokana na kuanzishwa kwa mfumo mpya wa njia ya pete.

Mfumo huo wa njia ya pete unatumia ngazi ya mafuta ya kupaka, hawatumii sindano na baada ya huduma hiyo mteja anaruhusiwa kuoga siku hiyo na atarejea kutolewa pete baada ya siku saba.

Mratibu wa huduma ya tohara hospitalini hapo, Haji Sued aliyabainisha hayo wakati akizungumza na Nipashe ofsini kwake juu ya namna wanavyopambana na ongezeko la maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) na UKIMWI kwa kundi la vijana na saratani ya shingo ya mlango wa uzazi kwa wasichana na kinamama.

Alisema baada ya mfumo huo kuanzishwa kundi kubwa linalojitokeza ni la watu wazima kulinganisha na kundi la vijana wenye umri wa miaka 15 na kuendelea na tayari watu 653 wamefanyiwa huduma hiyo kwa kipindi cha kuanzia Oktoba mwaka 2022 hadi Mei mwaka huu na bado wanaendelea kujitokeza.

Sued alisema kundi la vijana kwenye miaka 15 hadi 19 wamekuwa wakijitiokeza kipindi cha likizo za wanafunzi cha Aprili na Juni na wenye umri wa miaka 20 hadi 34 hujitokeza baada ya kipindi hicho kuisha.

Alisema njia wanayoitumia ili kuwafikia kwa wingi ni utoaji wa elimu kwa kinamama siku za kliniki, magulio na minada kwa kutumia kliniki tembezi, kwamba wanaojitokeza ni wengi.

Hata hivyo alisema mila na desturi potofu katika jamii bado ni tatizo kuwa huduma hiyo inapunguza nguvu za kiume jambo ambalo siyo kweli kwani inamkinga mtu kupata maambukizi ya VVU na Ukimwi kwa asilimia 60 na kumkinga mwenza na saratani ya shingo ya uzazi.

Baadhi ya wanufaika wa huduma hiyo akiwemo, Eva John aliyempeleka mtoto wake aliomba serikali kuendelea kutoa elimu ya huduma hiyo hususani maeneo ya vijijini pamoja na wanawake ili kusaidia kuwafikishia ujumbe wenza wao.



Ukurasa 12

**Jumuiya Wazazi yatangaza ujenzi benki, hospitali kikanda**



Ukurasa 13

Katiba mpya kwa maslahi ya wote ni sahihi, lakini...



Ukurasa 14

**Museveni shujaa harakati za 'no' ushoga, anapokwaa UVIKO-19**

siasa

JUMATANO JUNI 14, 2023

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

# Chama ACT-Wazalendo chaona jambo Muungano, katiba yatakiwa kulimaliza

## • Chataja makuu ya Samia, haijawahi tokea tangu 1964

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MAKAMU Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo, ambaye pia Makamu wa Kwanza wa Rais wa SMZ, Othman Masoud, anasema Zanzibar inahitaji mamlaka kamili ili kufunguka kiuchumi katika mfumo wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Anapohutubia mikutano ya ACT-Wazalendo, anasema mfumo wa sasa unainyima Zanzibar fursa ya kujiamulia mambo yake na kuwataka wananchi na viongozi wa Zanzibar kutumia fursa ya mchakato wa mabadiliko ya katiba kutetea mambo ya msingi yatakayonufaisha Zanzibar.

Aidha, anasema mchakato wa marekebisho ya katiba uliozishwa na Rais Samia ni fursa pekee ya kuondosha mambo yanayoikandamiza Zanzibar kiuchumi ndani ya muungano huo.

Othman anasema licha ya Rais Samia kutoa mabilioni ya fedha kwa ajili ya kupunguza makali ya UVIKO-19, vijana hawakuandaliwa kuitumia fursa hiyo.

Akizungumzia wazalishaji wa mazao ya chakula, anasema wameshindwa kunufaika na soko la sekta ya utalii kwa sababu serikali imeshindwa kuwawezesha ili kuinua uzalishaji wa mazao mbalimbali.

"Sekta ya utalii Zanzibar inategemea chakula kutoka Tanzania Bara kwa sababu wakulima wetu hawakuandaliwa lakini kama wangewezeshwa wangenufaika," anasema Othman.

Halikadhalika anasema asilimia 80 ya wafanyakazi katika sekta ya utalii wanatoka nje ya Zanzibar kwa sababu serikali haijawaandaa vijana wake kitaaluma tangu ilipoazishwa sekta hiyo na serikali ya awamu ya tano chini ya mstaafu Dk. Salmini Amaour Juma.



Ismail Jussa Ladhu, Mjumbe wa Kamati Kuu ya ACT- Wazalendo.

Othman anasema hatua hiyo ina madhara makubwa kwa sababu inasababisha mzunguko wa fedha Zanzibar kupungua na kusafirishwa nje wanakotoka wafanyakazi hao.

Anasema juhudi za kuondosha umasikini zinahitajika kwa vile vijana wingi Zanzibar wanakabiliwa na tatizo la ajira.

**SOKO HURIA KARAFUU**

Makamu huyo anaigeukia karafuu ambayo ni maarufu visiwani hapa akisema ni miongoni mwa mazao yanayochangia pato la taifa.

Anasema ACT-Wazalendo itaruhusu, soko huria kwa zao la karafuu muda mfupi watakaposhika madaraka kupitia uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 na kusema mfumo unaotumika hivi sasa mkulima kufanyakazi ya kuzalisha na serikali kuuza katika soko la nje si mwafaka na unachangia kurudisha nyuma maendeleo ya zao hilo.

Anasema historia inaonyesha Zanzibar ilikuwa inaongoza kwa uzalishaji wa karafuu kwa kuzalisha karibu tani 20,000 lakini uzalishaji umeshuka na kufikia tani kati ya 4,000 hadi 5,000.

Othman anasema hakuna njia nyingine ya kuendeleza karafuu zaidi ya zao hilo kuachiwa kuwa huria jambo ambalo litamaliza hata biashara ya magendo.

"Pamoja na serikali kufidia bei ya sasa kwa asilimia 80 wakulima bado kuna haja ya kuachiwa wenyewe wauze katika soko la nje badala ya wao kuwa wakulima na serikali kuwa wauzaji,"anasema.

Anaeleza kuwa gharama za uzalishaji wa karafuu ni kubwa na kutoa mfano pishi moja au kilo moja lina faida ya Shilingi 7,800 ukitoa malipo ya mchumaji na mkulima katika pishi hilo mkulima anabakia na 4,000 mbali na gharama za matayarisho ya vifaa vya kukaushia karafuu.

Karafuu daraja la kwanza hivi sasa inauzwa Shilingi 14,000 kwa kilo ambapo serikali ya awamu ya saba chini ya uongozi wa Dk. Ali Muhamed Shein, ilipandisha bei ya zao hilo kutoka Shilingi 10,000 kwa daraja la kwanza na kufikia 14,000.

**SAMIA JUU ZAIDI**

Wakati Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ukielekea miaka 60 tangu kuazishwa mwaka 1964 ACT-Wazalendo, inasema Rais Samia Suluhu Hassan, amefanya jambo ambalo halijawahi kutokea katika historia ya muungano huo.

Ismail Jussa Ladhu, mjumbe wa Kamati Kuu ya ACT Wazalendo, anasema Rais Samia ameipatia kiwango kikubwa cha mgao wa fedha za UVIKO-19 Zanzibar baada ya serikali kukopa katika Shirika la Fedha Duniani (IMF) ili kupunguza makali ya athari ya maradhi ya UVIKO-19 kwa taifa.

Jussa amekuwa akimwagia sifa Rais Samia kila anapohutubia mikutano ya hadhara ya chama hicho inayoendelea Zanzibar licha ya kuonyeshwa kukerwa na matumizi mabaya ya fedha hizo.

"Katika historia ya Muungano ni mara ya kwanza kupata mgao mkubwa wa fedha kama hizi ambazo Zanzibar imepatiwa bilioni 230 kwa ajili ya miradi ya maendeleo baada ya sekta za kiuchumi kuathiriwa na maradhi ya UVIKO-19,"anasema Jussa.

Tanzania ilikopa Shilingi trilioni 1.3 kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF) ili kukabiliana na ugonjwa wa UVIKO-19 kuelekea mwishoni mwa mwaka 2021.

Anaeleza kuwa Rais anapambania kuiletea nchi maendeleo bila ya kuuminya upande wowote wa Muungano ili kuhakikisha hali sawa kwa pande mbili hizo.

Aidha, anasema licha ya juhudi hizo za Rais Samia kutoa mgao wa fedha kuipatia Zanzibar lakini anasema kuna ubadhirifu mkubwa katika matumizi ya fedha hizo ambazo ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya SMZ na Serikali ya Muun-

**INAENDELEA UK. 12**

# Jumuiya Wazazi yatangaza ujenzi benki, hospitali kikanda

## •Mambo yote ndani ya miaka mitano

**Na Sabato Kasika**

KASI ya maendeleo katika nyanja mbalimbali imeifanya Jumuiya ya Wazazi ya CCM kuja na vipaumbele vinne ambavyo itavitekeleza katika kipindi cha miaka ijayo, ili kuwa na mchango kwa taifa.

Vipaumbele vya jumuiya ni ujenzi wa hospitali ya kanda, kuwa na benki, mashamba ya malisho ya mifugo na viwanda vya kuchakata matunda kwenye maeneo ambayo malighafi hizo huzalishwa kwa wingi.

Hayo ni kwa mujibu wa Mwenyekiti wa jumuiya hiyo taifa, Fadhil Maganya, katika mazungumzo na Nipashe yanayofanyika jijini Dar es Salaam, hivi karibuni akifafanua kuwa majukumu yao ni pamoja na kuhamasisha wazazi na Watanzania kuhusu muhimu wa elimu pamoja na kuanzisha na kusimamia shule za jumuiya.

"Kusimamia maadili na malezi bora kwa vijana na jamii kwa ujumla, ili kujenga taifa lenye maadili na linalosimamia misingi ya utamaduni wa Kitanzania,"anasema Maganya na kuongeza kuwa majukumu mengine ni kusimamia rasilimali pamoja na shughuli za kiuchumi zilizopo, na kubuni miradi mipya, kwa manufaa ya jumuiya na taifa kwa ujumla.

Sasa hapa ndipo tuliposimamia, hivyo tunakuja na vipaumbele vinne vya ujenzi wa hospitali, kuanzisha benki, kuwa na mashamba ya mifungo na ujenzi wa viwanda vya kuchakata matunda, kuzalisha nguo na magunia," anasema.

### UJENZI HOSPITALI

Mwenyekiti anasema Baraza Kuu la Jumuiya limeridhia ujenzi wa hospitali hiyo, na kwamba imepata eneo la heka 100 za kuanzia zilizopo Kazuramimba mkoani Kigoma akiongeza:"Wilaya hiyo imetupatia eneo hilo na tunategemea pia kuwa na chuo cha mafunzo ya mambo ya afya katika hospitali hiyo itakayogharimu zaidi ya Shilingi bilioni 20."

Aidha, wataongeza heka nyingine hapo baadaye kulingana na mahitaji yatakavyokuwa ili kuhakikisha malengo yao ya kutoa huduma za vyama na kuongeza wataalamu wa kada hiyo yanatimia, anaeleza.

“Unapokuwa na mtaji fanya mwenyewe, kama huna, ingia ubia au hisa ama pata ardhi na kuirasimisha, ita wale wanaotaka kushirikiana nawe, ndivyo tutakavyofanya hata kwenye ujenzi wa viwanda na uanzishaji wa mashamba ya malisho ya mifugo,” anasema.



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi CCM Taifa, Fadhili Maganya. **PICHA: MTANDAO**

Anafafanua kuwa hata kama ujenzi hautakamilika ndani ya miaka mitano ya uongozi wake, anaamini itakuwa imeanza kutoa huduma kwenye baadhi ya idara ikiwamo ya mama na mtoto na wagonjwa nje.

"Watu wanaweza kuhoji kwa nini Kigoma? Ni kwamba tumeangalia kanda ambayo haina hospitali ya kanda tukabaini kuwa ni Magharibi ndio maana ili kusaidiana na serikali kutoa huduma za afya," anasema.

### UJIO BENKI

Mwenyekiti Maganya anasema ili kuwa na benki wanahitaji mtaji wa Shilingi bilioni tano za kuanzia, na kwamba watakaribisha wawekezaji mbalimbali iya kuendesha benki hiyo.

"Binafsi nimefanya ushauri na wataalamu wabobezi wa Kitanzania kwenye mambo benki wanasema ni nilikuwa wapi kuanzisha, hivyo wananitia moyo nisonge mbele," anasema.

Anasema uanzishaji wa benki mradi unaoweza kufanyika ukawa na tija, na kwamba na wao kama jumuiya wameona uwe miongoni mwa vipaumbele vyao kwa miaka mitano ijayo.

Kada huyo wa CCM anataja eneo litakalojengwa benki hiyo itakayoitwa Wazazi Commercial Bank jijini Dodoma, kisha itakuwa na matawi katika majiji ya Arusha, Dar es Salaam, Mwanza na Mbeya.

"Unapokuwa na mtaji fanya mwenyewe, kama huna, ingia ubia au hisa ama pata ardhi na kuirasimisha, ita wale wanaotaka kushirikiana nawe, ndivyo tutakavyofanya hata kwenye ujenzi wa viwanda na uanzishaji wa mashamba ya malisho ya mifugo," anasema.

### KWENYE VIWANDA

Akizungumzie eneo hilo anasema ujenzi wa viwanda utafanyika kulingana na maeneo ambayo malighafi inapatikana ili kurahisisha usafirishaji wake kwenda viwandani, :"Mfano, viwanda vya kuchakata matunda tutajenga maeneo ambayo yanalimwa matunda, kiwanda cha kuchakata pamba kitajengwa sehemu inapolimwa kwa wingi hasa kanda ya ziwa," anasema.

Anasema kiwanda cha magunia kitajengwa mkonge unapozalishwa kwa wingi ili Jumuiya ya Wazazi iwe na mchango kwa maendeleo ya taifa na wananchi wake na kwamba mbali ya vipaumbele hivyo vinne, wana mpango wa kuboresha sekondari za jumuiya hiyo ikiwamo kuwa na chache ili zijiendeshe kwa ufanisi, kuingia ubia na pia kuzifanya kuwa vyuo vya kati.

Anasema jumuiya hiyo ina shule 71 za sekondari kote nchini, na kwamba kinachoendelea sasa ni kuangalia ni ngapi waziendeshe, ngapi waingie ubia na pia ngapi wageuze kuwa vyuo vya kati.

"Hivyo tunaendelea na mchakato ili kujua ni ngapi tutaziendesha na kwa sababu ipi na pia tunataka kujua ni ngapi tutaingia ubia na kwa sababu lakini pia ni ngapi zitakuwa vyuo vya kati na kwa sababu zipi," anasema.

Anafafanua kuwa mchakato huo ukikamilika, kila kitu kitakuwa wazi, kwa kuwa wamedhamiria kufanya maboresho mbalimbali katika jumuiya hiyo ikwamo kuwa na vipaumbele vinne alivyotaja.

# Chama ACT-Wazalendo chaona jambo Muungano, katiba yatakiwa kulimaliza

INATOKA UK. 11

gano wa Tanzania zimeanisha ubadhirifu huo.

"Kwa mujibu wa ripoti ya mdhibiti na mkaguzi mkuu wa serikali, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ilipatiwa Shilingi bilioni 2.3 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali katika sekta ya uvuvi lakini kuna ubadhirifu mkubwa katika pesa hizo," anadai Jussa.

Anaongeza kuwa cha kusikitisha fedha hizo zimetumika vibaya na nyingine hazieleweki matumizi yake na kutoa mfano wa zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa ya ufugaji samaki takribani milioni 132 mpaka sasa hakuna kilichojengwa, jambo ambalo ni kinyume na maelekezo ya matumizi ya fedha hizo.

"Rais Samia anatoa fedha hizi kusaidia sekta za kiuchumi baada ya kuathiriwa na korona lakini ripoti ya CAG Tanzania amefanya ukaguzi wa matumizi yake Zanzibar na kugundua madudu matupu kila pahala tunataka hatua za kisheria zichukuliwe," anadai Jussa.

# Katiba mpya kwa maslahi ya wote ni sahihi, lakini...

**Na Dk. Felician Kilahama**

KATIKA kuziangalia siasa za Tanzania kuna wakati nilizungumza kwa nini maslahi ya taifa hayazingatiwi? Kwenye kulitafakari kwa kina suala hili pia kwa kujadiliana na baadhi ya wadau na wananchi, inaonekana kwamba kwa Watanzania masilahi au faida binafsi zinafahamika zaidi.

Ingawa siyo lazima masilahi yafanane, lakini wengi wetu tunahitaji kuishi maisha yaliyo bora kupitia juhudi za kila siku pamoja na kipato cha mtu binafsi au familia kuweza kuishi vizuri. Kwa upande wa 'masilahi mapana' ya taifa letu, wengi ni 'kitendawili' hatuyajui ni yapi na yakoje.

Hata hivyo, tunaposema kuishi vizuri tunamaanisha nini? Wengi wanasema hali hiyo ni pamoja na kuwa na amani mioyoni, kwenye familia zetu, jamii na taifa pia.

Kadhalika, ilionekana binadamu aliye na maisha bora anapaswa awe na chakula cha kutosheleza mahitaji na chenye kukidhi afya ya mwili na akili. Aidha, huduma za jamii ziwe bora na rafiki kwa kila mtu, elimu, kazi, usafiri na usafirishaji viendane na mahitaji ya watu mijini na vijijini na rasilimali ardhi na maliasili zote vitumike kwa faida ya wote.

Hiyo ni pamoja na kusimamia vizuri nguzo kuu za 'uchumi wa taifa letu' mathalani, matumizi bora ya ardhi, kilimo, ufugaji, maliasili kama misitu, nyuki, wanyamapori, utalii, madini, maji, uvuvi, mafuta na gesiasilia bila kusahau viwanda, biashara ikiwamo shughuli za kibenki na huduma za bima, za kifedha mitandaoni na usafirishaji na kuhakikisha mazingira watu wanayoishi yanakuwa safi na salama kwa kuzingatia utupaji takangumu ovyo na kutiririsha majitaka mitaani vinakomeshwa.

Hayo yote yakifanyika kwa umakini mkubwa, alama ya maisha bora kwa Mtanzania itaonekana, ikiwamo haki, amani, furaha na upendo kwa wote. Katika kutafakari masuala hayo yote, ikadhihirika kwamba kuna vitu vya ziada ambavyo viko juu ya uwezo wa mtu binafsi na au jamii kwa ujumla. Hii ni pamoja na uboreshwaji wa huduma za kijamii ikiwemo, afya, elimu, maji, miundombinu, usafiri na usafirishaji, ugani kwa masuala ya kilimo, ufugaji, uvuvi, misitu na nyuki na maendeleo ya jamii.

Kwa kiasi fulani, mtu binafsi au jamii, inawezekana kujitahidi na kufanya kitu lakini haitafikia kiwango kinachotarajiwa. Hivyo, nguvu ya ziada zinahitajika kuboresha maisha ya wananchi na kuleta maendeleo kwa taifa zima.

Ikumbukwe chimbuko la kuwapo huduma zinazotakiwa kutolewa na serikali, ni kuboresha maisha ya kila mwananchi kwa kuzingatia 'masilahi mapana' kwa taifa lolote. Hii inamaanisha kuwepo na: "Siasa safi pamoja na utawala, uongozi bora" pamoja na misingi imara ya 'utawala



Baadhi ya wabunge wa lililokuwa Bunge la Katiba wakishiriki mijadala. **PICHA: MTANDAO**

> Kwa upande mwingine, iwapo nidhamu itakosekana na mambo yakafanyika kinyume na sheria, kwa lengo la kunufaisha wachache...

bora' ikawepo pia ikaheshimiwa na kuweza kutekeleza sheria, kanuni na taratibu kila wakati wa utendaji bila kusitasita.

Kwa upande mwingine, iwapo nidhamu itakosekana na mambo yakafanyika kinyume na sheria, kwa lengo la kunufaisha wachache, hata kama kutakuwepo na "katiba mpya," maisha bora kwa kila Mtanzania itabaki kuwa nadharia muda wote.

Kwa kuzingatia masuala ya kisheria inaoneka "katiba ya nchi" ndiyo msingi wa yote, ikijulikana kama "sheria kuu", mzaliwa wa kwanza, katika masuala ya utawala na uongozi wa nchi na kuhusika na mambo yote muhimu ya kitaifa. Hivyo, mambo muhimu kwa mustakabali wa taifa letu ni pamoja na 'masilahi mapana' kwa maishabora kwa kila Mtanzania.

Yanapotajwa maslahi ya taifa Watanzania tunayajua na kuyaelewa vizuri hayo masilahi ambayo kimsingi ndiyo faida kwa watu wengi? Iwapo tunayaelewa je, ni yapi yaliyozingatiwa kwenye katiba ya sasa (1977) au katiba pendekezwa?

> Hili ni jambo jema na la kupongeza sana hata hivyo, tuangalie pia na sekta nyingine kama misitu, nyuki na utalii ili vijana, wa kiume...

Nitoe rai kwa Watanzania hususani walio na kiu kuu ya kupata katiba mpya, watu wasidai katiba kulingana na matakwa yetu binafsi bali tutafute Katiba itakayobeba mustakabali na 'masilahi ya taifa zima hivyo kuweza kuyafikia maishabora kwa kila Mtanzania.

Tanzania ni taifa kubwa Afrika Mashariki, ikiwa na ardhi ya kutosha takribani zaidi ya hekta milioni 80, kuna watu zaidi ya milioni 60 na wengi wakiwa vijana. Kimsingi vijana ndiyo nguvukazi kubwa ya taifa hivyo vijana wasipotumika ipasavyo maendeleo ya nchi huwa duni.

Kimsingi, taifa lihakikishe vijana wanatumika ipasavyo na wajue wajibu wao bila kigugumizi, kwa kuzigatia 'maslahi mapana' ya nchi yetu iwajengee uwezo na kuwatia 'moyo wa uzalendo' na dhamira thabiti ya kuliendeleza taifa lao.

Tukiwekeza kwa kusudio la kuwapatia vijana wetu ajira za kutosha, utegemezi wao kwa wazee utaisha na wao watakuwa msaada mkubwa kwa vijana wengine pia. Nashukuru Serikali imeanza kuchukua hatua kupitia miradi ya kimkakati katika sekta za kilimo na mifugo na kuwahusisha zaidi vijana.

Hili ni jambo jema na la kupongeza sana hata hivyo, tuangalie pia na sekta nyingine kama misitu, nyuki na utalii ili vijana, wa kiume na kike, wakiwezeshwa sawa sawa watafanya makubwa na taifa litapiga hatua kimaendeleo.

Tunapofanya hivyo mkazo uelekezwe kwenye masuala yenye masilahi ya taifa, yenye kuinua maisha ya wengi na taifa kwa ujumla, kuwa na maendeleo endelevu. Vijana wengi kuendelea kuwategemea wazee wao ni janga kubwa kijamii na kitaifa.

Hivyo, vijana wetu mijini na vijijini wahimizwe, watiwe moyo na kwa weledi mkubwa na maarifa, wafanye kazi kwa nguvu zao zote kwa faida ya wengi. Tulio madarakani tusifikirie nafsi au nyadhifa zetu bali tujichimbie zaidi katika kuyafanikisha manufaa ya nchi na yenye kuwaletea maendeleo Watanzania wote tukizingatia matumizi sahihi ya nguvu za vijana.

Kwa hiyo vijana wa kiume na kike wapewe fursa sawa na wafanye kazi kwa kujituma kwa faida ya wote huku wakizingatia umoja na mshikamano wa kitaifa. Haya yakizingatiwa, pamoja na uwepo wa siasa safi na uongozi bora, tunaweza kusonga mbele ndani ya muda mfupi. Je, ni mambo gani zaidi yenye umuhimu wa pekee kuweza kufanikisha na kupata matokeo yanayobeba masilahi ya Tanzania?

Wakati umefika kwa Watanzania wengi kufafanua maeneo muhimu takriban matano yenye mwelekeo wa kubeba mustakabali mzima na masilahi ya nchi yakiainishwa na kukubaliwa na wengi yaingizwe kwenye katiba, upatikane msingi au nguzo kwa matumizi sahihi ya rasilimali zetu na serikali itayokuwa madarakani ielekeze nguvu zake huko.

Kila kitakachofanyika msingi wake uwe kwenye maeneo yaliyoainishwa na kukubalika na Watanzania wengi kwa faida ya wote.

# Museveni shujaa harakati za 'no' ushoga, anapokwaa UVIKO-19



Rais Museveni (mwenye barakoa nyeupe), pamoja na Rais wa Somalia, Hassan Sheikh Mohamud, walipokuwa Ikulu ya Entebbe Agosti mwaka jana. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Yoweri Museveni (78) wa Uganda ametangaza kuwa ameambukizwa COVID-19, wakati kiwango cha maambukizo kimepungua nchini humo na duniani pia.

Tangazo lake linaibua maswali mengi. Pengine kuna watakaofikiri kuwa kuna mkono wa mtu na huenda 'ametupiwa' maradhi hayo kutokana na katazo la vitendo vya ushoga na kutunga sheria inayoadhibu kwa kifungo na hata kunyonga mashoga na wanaojihusisha na kuendeleza au kuunga mkono mambo hayo.

Wiki iliyopita Museveni anasema alijisikia mafua myepesi na pua moja ya kulia ikibana kiasi na akapuuza hata hivyo hali ilizidi kuwa mbaya na akaamua kupimwa matokeo yake akawa na COVID- 19, hivyo kuanzia Alhamisi iliyopita alichukua likizo ya lazima na kuacha madaraka na uongozi wa nchi kwa Waziri Mkuu mwanamama Robinah Nabanja.

Museveni ni kiongozi ambaye siku zote amepigana na COVID-19 au UVIKO-19 nje na ndani ya Uganda. Tena akivaa barakoa muda wote, lakini karibuni akaeleza kuwa ameamua kuziacha kwa sababu zilikuwa zikimsababishia mzio au aleji machoni na kooni na kuanza kupata tena usumbufu mwingine kiafya, linaeleza gazeti la The Monitor.

Ni kwa mara ya kwanza anatupa barakoa, linaongeza The Monitor, lakini hata hivyo ameendelea kujitenga na mikusanyiko, kutumia vitakasa mikono na kuchukua tahadhari zote akikaa mbali na kujihakikishia kuwa haambukizwi. Safari hii mambo yakamgeukia ndiyo maana huenda wapo wanaotaka kumuonya kuwa akae chonjo.

> Museveni ni Rais wa shoka aliyesema ya moyoni, kwani ushoga Afrika unaonekana kuwa ni kinyume cha sheria na watu wa LGBTQ hawakubaliki.

### KUPINGA USHOGA

Ni kiongozi pekee Afrika aliyesimama hadharani na kusema hakubaliani na kampeni za kuendeleza na kubariki uhusiano wa jinsia moja akiamua kutunga sheria kali bila kujali vitisho na kelele za mataifa ya Marekani, Ulaya na wahisani wa Afrika wa magharibi ambao wanatetea mambo hayo wakieleza kuwa ni haki za binadamu.

Hata katika ziara ya Makamu wa Rais wa Marekani iliyomfikisha pia Tanzania mapema mwaka huu, Makamu Kamala Harris alitangaza kuwa Marekani iko pamoja na inawaunga mkono Waafrika wanaojihusisha na ngono za jinsia moja wanaume (mashoga), wasagaji kwa wanawake, watu wa jinsia mbili, waliobadilishwa jinsi, wasio na jinsi zote ambao kwa kifupi huitwa ' LGBTQ+'.

Bila kusita anasema Marekani inawaunga mkono licha ya kuanzishwa kwa sheria mpya anayoiita mbaya nchini Uganda ambayo inapiga marufuku utambulisho na kujiifaharisha kushiriki ushoga.

Makamu huyo wa Rais wa 49 Marekani anaweka msimamo wake wazi Jumatatu Machi 27,2023 huko Accra wakati wa mkutano na wanahabari.

Hata hivyo Bunge la Ghana lilimpinga baada ya kulihutubia na kutoa wito wa 'usawa na uhuru wa watu wote bila kubagua LGBTQ+.

Licha ya Marekani kutoa kauli kali za kulaani na kukosoa Uganda, Museveni 'aliinjinia' au kusimamia kidete uwepo wa adhabu na kukomesha mienendo ya uhusiano wa jinsia moja ndipo Uganda inapotunga na kupitisha sheria inayoharamisha ndoa na mapenzi ya jinsia moja, ikiwa ni pamoja na adhabu ya hadi miaka 10 jela na faini ya hadi Shilingi milioni 10 za Uganda sawa na Shilingi 6,000,000 za Tanzania.

Sheria hiyo pia inatoa adhabu ya kifo kwa "ushoga uliokithiri," kosa ambalo ni pamoja na kusambaza UKIMWI kupitia ngono ya mashoga. Aidha, sheria pia unawabana watu wanaoshiriki mapenzi ya jinsia moja, wamiliki wa nyumba za wageni na hoteli wanaotetea ushoga, wamiliki wa vyumba vya burudani, waandishi wa habari, watengenezaji filamu na wote wanaopigia debe ushoga.

Adhabu kwa wanaoeneza habari za ushoga kwa kuchapisha vitabu pamoja na wafadhili watatozwa faini ya Shilingi milioni 100 za Uganda sawa na Shilingi milioni 64 za Tanzania.

Wanaomiliki vyumba vya kufanyia ushoga watahukumiwa miaka saba jela wakati wamiliki wa nyumba watakaokodisha kwa mashoga watahukumiwa mwaka mmoja gerezani.

Rais Museveni aliusaini muswada huo wenye adhabu kali dhidi ya watu wanaojihusisha na mapenzi ya jinsia moja kuwa sheria ya ushoga ya mwaka 2023 baada ya kufanyiwa marekebisho ambayo vipengele vingi vyenye msimamo mkali vimebakizwa.

Taarifa iliyochapishwa kupitia akaunti rasmi ya Twitter ya Rais huyo wa Uganda wakati huo ilieleza kuwa amekubali muswaada wa kupinga mapenzi ya jinsia moja wa mwaka 2023, sasa unakuwa sheria ya kupambana na mapenzi ya jinsia moja 2023.

Kadhalika, bunge la Uganda nalo likakoleza kupitia ukurasa wake wa Twitter likisema wabunge wamechukua hatua hiyo ili kulinda utamaduni na maadili ya taifa hilo.

Rais wa Uganda ambaye hafanyi ajizi alianza mwaka huu kwa kuwapasha mashoga na ilikuwa ni ujumbe alioutoa Machi mwaka huu, akiwaelezea kuwa ni "wapotovu" na "ni mwenendo wa tabia unaokiuka maadili", akisisitiza kuwa mambo hayo hayakubaliki.

Uhusiano wa watu jinsia moja unakubalika katika mataifa machache kati ya 54 ya Afrika. Baadhi ya nchi, sheria zinaimarishwa dhidi ya watu wanaojitambulisha kama LGBTQ, na wanaonekana kama wanakwenda kinyume na kanuni za kitamaduni.

Museveni ni Rais wa shoka aliyesema ya moyoni, kwani ushoga Afrika unaonekana kuwa ni kinyume cha sheria na watu wa LGBTQ hawakubaliki.

Karibu nusu ya nchi zote duniani ambako ushoga umeharamishwa ni barani Afrika, kulingana na mapitio ya kimataifa ya chama cha kimataifa cha wasagaji, mashoga, wenye jinsi mbili -ILGA (the International Lesbian, Gay, Bisexual, Trans and Intersex Association).

Kwa ujumla Museveni amewekа wazi kile ambacho Waafrika wengi wanakichukia na kuwachukulia mashoga kama wageni wenye tamaduni za Kimagharibi.

### MAREKANI KUFOKA

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, akawaka akisema Marekani inawawekea vikwazo baadhi ya maofisa wa Uganda baada ya nchi hiyo kupitisha sheria kali zaidi duniani dhidi ya LGBTQ.

Sheria ya Ushoga Uganda ifutwe haraka - Biden ni kichwa cha habari cha Sauti ya Amerika (VOA).

Kilichofuata Mei 30, 2023 ni Rais wa Marekani, Joe Biden, kuishutumu sheria mpya ya Uganda inayopinga mapenzi ya jinsia moja na kusema kuwa inakiuka haki za binadamu, na inahatarisha maendeleo ya uchumi wa nchi hiyo.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari, Rais Biden analaani hatua hiyo ya kuanzishwa sheria inayoharamisha mapenzi ya jinsia moja, ikiwa pamoja na adhabu ya hadi miaka 10 jela na faini ya hadi shilingi milioni 10 za Uganda na kifo.





## TBS yatoa elimu sumukuvu kwenye mazao ya nafaka

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) limeendelea kutoa mafunzo ya udhibiti wa sumukuvu kwenye mahindi, karanga na bidhaa zake katika Wilaya ya Kiteto, Kongwa, Gairo na Kilosa.

Mafunzo hayo yamewafikia wasafirishaji, wafanyabiashara na wasindikaji wa mahindi na karanga zaidi ya 600, yameanza Mei 31 na yatahitimishwa Juni 14, mwaka huu.

Mafunzo hayo yanatolewa na shirika hilo kupitia Mradi wa Kitaifa wa Kudhibiti Sumukuvu uitwao TANIPAC.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa mafunzo hayo Jabir Abdi, ambaye ni Mwenyekiti wa mradi huo kutija TBS alisema mafunzo hayo yatawasadia wafanyabiashara na wasindikaji wa mahindi na karanga kupata masoko ya uhakika na kuwezesha wananchi kuepukana na madhara ya kiafya yatokanayo na sumukuvu.

Alisema mafunzo hayo yametolewa kwenye wilaya hiyo kutokana na utafiti wa awali za mradi huu kubaini kwamba wilaya hizo kuwa miongoni mwa maeneo yenye matatizo ya uwapo wa sumukuvu katika mnyororo wa thamani wa mazao ya mahindi, karanga na bidhaa zake.

Abdi alitaja faida za mafunzo kuwa yalenga kulinda afya za binadamu, kuwezesha biashara ya mazao ya mahindi na karanga, kulinda afya za mifugo na kuwezesha utoshelevu wa chakula salama.

Kwa mujibu wa Abdi faida nyingine za mafunzo hiyo ni kuwawezesha wadau katika mnyororo wa karanga, mahindi na bidhaa zake kuhimili ushindani katika masoko ya ndani, kikanda na nje ya nchi.

Alifafanua kwamba mafunzo hayo ni muhimu kwa sababu usalama wa chakula unakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na uchafuzi wa sumukuvu ambao husababisha madhara ya kiafya na hata kiuchumi.

Alisema sumukuvu huathiri zaidi mazao ya mahindi na karanga ambayo ni sehemu muhimu ya chakula cha Watanzania hapa nchini.

"Kwa sababu hiyo sisi sote tunatakiwa kuzingatia mikakati ya kukabiliana na sumukuvu ili vyakula vyetu viendelee kuwa salama kwa muda wote," alisisitiza Abdi.

Alifafanua kwamba TBS inatambua nafasi ya wafanyabiashara, wasindikaji na wasafirishaji kwa ujumla na mchango walionao, hivyo TANIPAC imeandaa mafunzo hayo mahususi kupitia TBS ili kuwajengea uwezo kwa ajili ya udhibiti sumukuvu.

Alisema umuhimu huu unasababisha suala la usalama wa chakula kupewa kipaumbele katika kulinda afya, jamii na uchumi wa nchi, kwa kuwa ndiyo kigezo muhimu cha biashara kitaifa na kimataifa.

# Kazi za ndani, migodini kinara kwenye utumikishaji watoto

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAKAMU Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Tanzania (THBUB), Mohamed Khamis Hamad, amesema kazi za ndani, shambani, mitaani na migodini ni sehemu zinazoongoza kwa utumikishwaji wa watoto nchini.

Amesema hali hiyo imekuwa ni kichocheo cha ukatili dhidi ya watoto, kwamba baadhi yao hukosa masomo, kunyonywa kiuchumi kwa kulipwa ujira mdogo na matatizo ya kiafya jambo linaloathiri ukuaji wao.

Aliyasema hayo juzi jijini hapa alipokuwa akitoa tamko la tume hiyo kwa waandishi wa habari wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kupinga Ajira kwa Watoto.

"Tume inatambua na kuunga mkono juhudi mbalimbali zinazochukuliwa na serikali katika kutokomeza ajira kwa watoto ikiwa ni pamoja na kuridhia mikataba ya kikanda na kimataifa.

"Kutunga sera na sheria ya mtoto ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ya Zanzibar ambapo zinakataza mtoto kuhusishwa katika kazi yoyote itakayoweza kumsababishia madhara kiafya, kielimu, kiakili, kimwili na katika ukuaji wake," alisema.

Alisema pamoja na jitihada hizo bado zipo kasoro mbalimbali ikiwamo watoto kuendelea kufanyishwa kazi ngumu katika maeneo ya kazi za ndani, shambani, mitaani na migodini.

"Ajira hizi zimekuwa kichocheo cha ukatili dhidi ya watoto ambapo baadhi yao hukosa masomo, kuminywa kiuchumi kwa kuwa hulipwa ujira mdogo na matatizo ya kiafya jambo linaloathiri ukuaji wao," alisema.

Vile vile, alisema miongoni mwa sababu zinazoendelea kuchangia ajira kwa watoto ni pamoja na umaskini na jamii kukosa uelewa juu ya madhara ya ajira hizo hali ambayo inasababisha watoto kufanya kazi ngumu ili kujikimu.

"Kupitia kaulimbiu ya mwaka huu, THBUB inaendelea kuhamasisha jamii kuheshimu haki za binadamu katika masuala ya kazi na ajira, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, sheria, sera na miongozo mbalimbali," alisema.

Alisema pia THBUB inatoa wito kwa serikali, wadau na jamii kuunganisha nguvu kupinga ajira kwa watoto mahali popote nchini.

Kadhalika, alisema tume inapendekeza serikali kuendelea kuhamasisha hatua za kimataifa kufikia haki ya kijamii na kuondoa ajira kwa watoto kama moja ya mambo yake muhimu.

"Serikali iendelee kuhakikisha kuwa suala la kutokomeza tatizo la ajira kwa watoto linapewa kipaumbele katika utengenezaji wa sera, shughuli za kitaifa na kimataifa, katika ushirikiano wa maendeleo na katika mikataba ya kifedha biashara na uwekezaji," alisema.

Hata hivyo, alisema jamii iendelee kutoa ushirikiano kwa kuwafichua watu wote wanaowaajiri na kuwatumikisha watoto na wazazi, kwamba walezi wahakikishe wanatunza, kuwalinda na kuwapatia watoto mahitaji yao ya msingi.



Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, akifungua bomba la maji kuzindua mradi wa maji wa Kijiji cha Iglansoni wilayani Ikungi hivi karibuni. Kulia ni Mkuu wa wilaya hiyo, Thomas Apson. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# TRA yaagizwa kuzingatia sheria wanapokusanya kodi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, ameiagiza Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuzingatia sheria zinapotekeleza majukumu ya ukusanyaji kodi kwa wafanyabiashara.

Alitoa agizo hilo jana wakati akifungua mkutano wa Baraza la Biashara la Mkoa wa Singida, kuwataka wafanyabiashara mkoani hapa kuzingatia miongozo ya ulipaji kodi wanazostahili kulipa na utoaji wa stakabadhi za kielektroniki ili kukuza uchumi wa mtu mmoja na taifa kwa ujumla.

Serukamba alisema serikali imekuwa ikiboresha mazingira ya biashara kwa kuondoa tozo ambazo hazina tija ili kuongeza ukuaji wa biashara na uwekezaji hivyo wafanyabiashara waunge jitihada hizi za serikali kwa kulipa kodi.

Alisema serikali pia imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kuhakikisha kuwa sekta za biashara na uwekezaji zinakuwa na kutoa mchango stahiki katika kukuza uchumi na pato la taifa kwa manufaa ya Watanzania.

Serukamba aliongeza kuwa ili kuhakikisha uboreshaji huu unakuwa na tija zaidi serikali imeanzisha idara ya uwekezaji, viwanda na biashara katika sekretarieti za mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kusimamia kwa karibu tasnia ya biashara nchini.

Alisema Mkoa wa Singida umebarikiwa kuwa na rasilimali nyingi hivyo sekta za umma na binafsi zinapaswa kufanya kazi kwa pamoja ili kuwaletea wananchi maendeleo na hivyo kukuza uchumi.

"Ndoto yangu ni kuifanya Singida kuwa kitovu cha biashara na uwekezaji nchini na chombo muhimu kitakachonisaidia kutimiza ndoto hii ni Baraza la Biashara la Mkoa hivyo tuweke mpango mkakati wa kufanya kazi ndani ya miaka mitatu kwa kutangaza shughuli za biashara na uwekezaji," alisema.

Aliongeza kuwa dunia kwa sasa inakabiliwa na mabadiliko makubwa ya teknolojia ambayo yanasababisha kukua kwa haraka kwa uchumi, hivyo jitihada zinahitajika kujipanga kukabiliana nazo kwa kuimarisha mazingira wezeshi ya wafanyabiashara.

"Kasi hii ya ukuaji wa teknolojia imeendelea kuibua matatizo mbalimbali katika mazingira ya biashara ambazo zinahitaji utatuzi kwa njia ya majadiliano kuzipitia ufumbuzi changamoto zote zinazokabili ufanyaji wa biashara kwa kuzingatia miongozo iliyopo," alisema Serukamba.

Naye Mwenyekiti wa Chemba ya Wafanyabiashara Wenye Viwanda na Kilimo (TCCIA) Mkoa wa Singida, Kitila Katala, alisema sekta binafsi imekuwa ikikabiliwa na mamlaka nyingi za udhibiti ambazo hudai tozo zaidi ya 18 na hivyo kuongeza mzigo mkubwa kwa wafanyabiashara.

Alisema serikali iweke utaratibu kwamba tozo zote hizo zilipwe kwa mamlaka moja ili kupunguza mtafaruku na kuwepo majadiliano badala ya kutumia nguvu katika kutekeleza majukumu.

"Mfano hivi karibuni hapa Singida wafanyabiashara waliofungiwa biashara zao kwa kudaiwa tozo ya huduma bila hata kupatiwa muda wa kunieleza ili wakubaliane cha kulipa," alisema Katala.

Kuhusu mashine za kielektroniki alisema zina ukomo wa kutumia ambapo wafanyabiashara wamekuwa wakitumia fedha nyingi kuzifanyia ukarabati na kuiomba serikali kama itawezekana mzigo wa kuzikarabati uwe unafanywa na TRA.

Kwa upande wake Ofisa Biashara kutoka Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania, Herbert Hatibu, alisema wafanyabiashara wanapaswa kushirikiana na mamlaka hiyo katika kutangaza biashara zao kupitia maonyesho biashara ambayo yamekuwa yakiandaliwa na TanTrade.





# Jeshi la Polisi lapewa saa 72 kuwasaka waliomjeruhi M/kiti

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

JESHI la Polisi wilayani Mbarali katika Mkoa wa Mbeya, limepewa saa 72 kuwasaka na kuwasweka ndani wafugaji wanaodaiwa kumvamia na kumjeruhi kwa kutumia silaha za jadi Mwenyekiti wa Skimu ya Umwagiliaji ya Uturo, Kandreza Kilongo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alitoa agizo hilo juzi alipofanya ziara ya kukagua ukarabati wa Skimu ya Umwagiliaji ya Uturo ambayo ni miongoni mwa skimu zinazochangia kwa kiwango kikubwa uzalishaji wa mpunga.

Akiwa katika eneo hilo, Homera alipata taarifa kuwa wafugaji jamii ya kimaasai walimvamia mwenyekiti wa skimu hiyo, Kandreza Kilongo.

Katibu wa Skimu hiyo, Jafar Mwinjuma alisema wafugaji hao walimshambulia mwenyekiti huo alipokuwa anawazuia kuingiza mifugo kwenye shamba lake la mpunga.

Alisema wafugaji hao walimshambulia na kumjeruhi na hivyo akaiomba serikali kuwashughulikia wafugaji hao kutokana na kuwasababishia wakulima hasara mara kwa mara.

"Walimjeruhi mwenyekiti wetu bila kosa, wao ndio walikuwa na makosa maana waliingiza mifugo kwenye shamba lake na alipokuwa anawazuia ndipo walimvamia na kuanza kumpiga," alisema Mwinjuma.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Homera aliagiza watu hao wasakwe na kuchukuliwa hatua kali za kisheria ili iwe fundisho kwa wengine wenye tabia hiyo.

Aidha aliagiza viongozi wa serikali katika wilaya hiyo kushughulikia migogoro ya wakulima na wafugaji haraka kabla haijaleta matatizo.

Vilevile aliagiza mashamba ya wakulima kuzungushiwa wigo ili kuzuia mifugo kuingia na kuharibu mazao hasa watakapokuwa wamemaliza ujenzi wa mifereji.

"Hili tatizo lazima lifike mwisho, watafuteni wafugaji hao na wawekwe chini ya ulinzi ili hatua zichukuliwe, hatuwezi kuwavumilia watu wanaoharibu chakula kwa makusudi halafu wanapiga wenzao," alisema Homera.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Kanali Denis Mwila, alisema baada ya wafugaji hao kumjeruhi mwenyekiti huyo alichukuliwa na kupelekwa hospitalini kwa ajili ya kupatiwa matibabu na kwamba kwa sasa anaendelea vizuri.

Alisema mara nyingi wafugaji hao wamekuwa ni wakorofi kutokana na kuingiza mifugo kwa makusudi kwenye mashamba ya wakulima na hivyo kuharibu mazao.

Alisema wataendelea kushughulikia migogoro ya aina hiyo ili kuhakikisha wananchi wanafanya shughuli zao bila kuingiliana na bila kuingia kwenye migogoro ambayo inavuruga amani.



Diwani wa Kata ya Ijombe wilayani Mbeya, Mary Mbengale (kushoto), akizungumza na wakazi wa kata hiyo, kwenye mkutano wa hadhara ulioandaliwa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Beno Malisa (hayupo pichani), uliohusu masuala mbalimbali yakiwamo ya ushiriki shughuli za maendeleo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wananchi wagoma kushiriki shughuli za maendeleo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI wa Kata ya Ntangano katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wamegoma kushiriki shughuli za maendeleo ikiwamo ujenzi wa shule na vituo vya afya hali inayoifanya kata hiyo kuwa na maendeleo hafifu.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Mwalingo Kisemba, aliyasema hayo wakati wa ziara ya Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa ya kukagua miradi ya maendeleo katika Kata ya Tembela na Ijombe.

Katika ziara hiyo Malisa alikagua ujenzi wa bwalo katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Garijembe lililogharimu zaidi ya Sh. milioni 200 pamoja na ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Shule ya Sekondari Iwalanje.

Mwalingo alisema katika halmashauri hiyo wananchi wanajitolea kufanya shughuli za maendeleo isipokuwa kata hiyo ya Ntangano ambayo wananchi wake ni wavivu lakini wanapata huduma muhimu kwenye kata za jirani.

Alisema wananchi hao wanakataa kujenga shule ya sekondari lakini watoto wao wanasafiri umbali mrefu kwenda kusoma katika Shule ya Sekondari ya Iwalanje ambayo ipo katika Kata ya Ijombe.

"Haiwezekani watu wakawa wavivu hawataki kujenga shule lakini watoto wao wanakuja kusoma huku, sasa wanataka nani awajengee, kwa hiyo tunakuomba Mkuu wa Wilaya ikiwezekana utusaidie hili jambo," alisema Kisemba.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Malisa aliagiza Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo kutembelea kata hiyo ya Ntangano na kuzungumza na wananchi hao ili kubaini sababu ya kugoma kufanya maendeleo.

Alisema endapo itabainika kuwa sababu za kugoma kushiriki shughuli hizo hazina mashiko serikali itaingilia kati na kuwalazimisha kushiriki.

Alisema shughuli za maendeleo ambazo wananchi hao wanatakiwa kushiriki ni kwa faida yao wenyewe na siyo faida ya serikali wala kiongozi yeyote.

Alisema kama ni shule inajengwa inakuwa ni kwa ajili ya watoto wa eneo husika na kama ni zahanati ama kituo cha afya kinajengwa wananchi wa eneo husika ndio wanaokuwa wananufaika kwa kutibiwa.

"Hapa nyie mnajenga shule yenu na wao wanatakiwa kujenga ya kwao, sasa hebu fuatilieni ili tujue sababu za wao kugoma kufanya shughuli hizo," alisema Malisa.

Vilevile aliwataka wananchi wa kata zote za wilaya hiyo kuhakikisha wanadai mikutano ya kusomewa mapato na matumizi ya fedha wanazopelekewa na serikali kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Diwani wa Kata ya Ijombe, Mary Mbengale aliwaomba wananchi wa kata hiyo kuhakikisha wanachangia chakula cha mchana kwa ajili ya watoto wao wanapokuwa shuleni ili kuongeza ufaulu kwenye mitihani mbalimbali.

Alisema kata hiyo imekuwa ikiburuta mkia mara kwa mara kwenye mitihani hasa kwa shule za msingi kutokana na kutokuwa na mikakati mizuri hasa kuchangia chakula cha mchana.

Alisema wamefuatilia na kubaini kuwa baadhi ya kata ambazo zinawashinda ikiwamo Kata ya Inyala ambayo ni jirani zinafanya vizuri kutokana na ushirikiano mzuri kati ya walimu na wazazi ikiwamo uchangiaji wa chakula.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Malisa anaendelea na ziara katika kata mbalimbali za wilaya hiyo kwa lengo la kukagua na kuhamasisha shughuli za maendeleo.

## Wakulima waomba adhabu wanaofunga lumbesa iongezwe

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

WAKULIMA wa viazi wa Tarafa ya Matamba wilayani Makete katika Mkoa wa Njombe, wameiomba serikali kupandisha kiwango cha adhabu kwa wanunuzi wa zao hilo kwa kutumia vipimo visivyoruhusiwa ikiwamo 'lumbesa' ili kudhibiti biashara hiyo.

Wananchi hao wanadai kuwa Halmashauri ya Makete imeweka adhabu ya Sh. 500,000 kwa mfanyabiashara ambaye anakutwa amezidisha uzito adhabu ambayo wanasema haitoshi kuwadhibiti wafanyabiashara hao.

Mmoja wa wakulima hao, Frank Mbwilo alisema wafanyabiashara hao hawaogopi adhabu hiyo na hivyo wanaendelea kuwanyonya wakulima jambo ambalo alisema halistahili kuendelea.

Alisema ili kuwadhibiti adhabu hiyo inatakiwa kuongezeka na kufikia zaidi ya Sh. 5,000,000 ili wafanyabiashara wawe wanaogopa kupata hasara endapo wataendelea kununua zao hilo kwa kutumia vipimo hivyo.

"Adhabu ya sasa hawaiogopi, wakikamatwa wanalipa na wanaendelea na safari, lakini tunaamini kwamba ikiongezeka watakuwa wanaogopa," alisema Mbwilo.

Naye Vangiles Mbwanji alisema wakulima wamekuwa wakiingia hasara kutokana na vipimo vinavyotumiwa na wanunuzi wa viazi hivyo.

Alisema mkulima anayekataa kuuza mazao yake kwa kutumia vipimo hivyo wanagoma kununua mazao yake na hivyo kusababisha wakulima wengi kuingia mkenge na kuwauzia.

Alisema wakulima huwa wanalazimika kuuza kwa kutumia vipimo hivyo kwa sababu wakati mwingine wanakuwa wanadaiwa na taasisi za kifedha.

Baadhi ya madereva wa magari ya kubeba viazi walisema wao huwa hawahusiki na badala yake wanaohusika ni wanunuzi lakini wanaposafirisha wao ndio hukamatwa na kutakiwa kulipa faini.

Hata hivyo alisema wanapokamatwa huwa wanawasiliana na wanunuzi ambao ndio wanakuwa wamiliki wa mizigo ambao hulipa adhabu na kuruhusiwa kuendelea na safari.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Maketa, William Makufwe alisema waliamua kuweka utaratibu huo wa kuwatoza faini ili kukomesha biashara hiyo inayowanyonya wakulima.



## Serikali kutumia matokeo ya sensa kupanga maendeleo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema matokeo ya taarifa za Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 zitatumika kwa ajili ya mipango ya maendeleo ya bajeti ya serikali kwa mwaka wa fedha 2023-2024.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya Salum, alisema hayo jana wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2023-2024 katika kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Dk. Mkuya alisema taarifa zote za matokeo ya sensa zimewasilishwa kwa serikali ya mapinduzi ya Zanzibar ambapo tayari wizara zote zimepatiwa kwa ajili ya kuzijumuisha na taarifa zao.

Aidha alisema katika bajeti ya serikali inayotarajiwa kuwasilishwa Juni 15, mwaka huu taarifa hizo zimo na zitawasilishwa.

Waziri huyo alisema taarifa hizo zitasaidia katika mipango ya maendeleo katika halmashauri za serikali za mitaa katika utekelezaji wa majukumu kwa mujibu wa idadi ya watu ilivyo.

Hata hivyo alisema serikali tayari imekamilisha utafiti muhimu zinazoonesha hali ya maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI pamoja na kujuwa tatizo la vifo vya kinamama na watoto.

Alisema utafiti wa viashiria na matokeo ya ugonjwa wa UKIMWI ni muhimu ambao utaiwezesha serikali kufahamu hali ya ugonjwa huo na hadi Machi mwaka huu kazi ya kukusanya taarifa za viashiria vya ugonjwa huo umekamilika ambapo jumla ya watu 4,000 walihojiwa.

# ACT-Wazalendo: Majengo hospitali 12 yanakasoro

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema majengo mapya 12 ya hospitali 11 za wilaya na moja ya mkoa visiwani Zanzibar yamejengwa chini ya kiwango, ikiwamo vyumba vya kufunga mashine za uchunguzi kuta zake kutokuwa na uwezo wa kudhibiti mionzi ya mashine ya X-ray, kwamba mionzi hupenye nje na kuleta athari.

Hayo yalielezwa na Mjumbe wa Kamati Kuu wa chama hicho, Ismail Jussa Ladhu, wakati akihutubia mkutano wa hadhara katika viwanja vya Mjimbini Kisiwani Pemba.

"Tunazo taarifa kati ya hospitali zilizojengwa kuna vyumba vimejengwa chini ya viwango vya ubora na mashine za uchunguzi kama X-ray haziwezi kutumika kwa sababu mionzi inauwezo wa kupenya kuta na kuleta madhara kwa wananchi," alisema Jussa.

Aidha, alisema kwa mujibu wa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Wizara ya Afya iliidhinisha kununua magari 12 ya kubeba wagonjwa kupitia fedha za UVIKO-19 lakini hadi ukaguzi unakamilika hakuna gari iliyonunuliwa.

Jussa alisema Rais Samia Suluhu Hassan alikuwa na nia njema ya kusaidia Zanzibar kutokana na sekta za kiuchumi kuathirika na maradhi hayo lakini bahati mbaya fedha hizo zimevurugwa na hatua za kisheria zinapaswa kuchukuliwa kwa watu waliohusika.

Alisema gari hizo za kubeba wagonjwa zilitengewa Sh. bilioni 1.9 ili hospitali za wilaya zilizojengwa zitoe huduma bora ya kuwahudumia wagonjwa kutokana na eneo moja kwenda lingine hasa ikizingatiwa maeneo mingi ya vijijini hasa nyakati za usiku huduma za usafiri hakuna.

Aidha, alisema kwamba wanazo taarifa kuwa kuna mpango wa kubinafsisha huduma za uchunguzi wa vipimo katika hospitali za serikali na kupewa kampuni binafsi kuendesha shughuli hizo.

"Tunazo taarifa shughuli za uchunguzi wa vipimo kuna mpango wa kupewa kampuni binafsi inakuaje mashine za serikali unaipa kampuni binafsi uendeshaji ikusanye mapato wakati serikali ndio yenye wajibu wa kutoa huduma za afya kwa wananchi wake kwa mujibu wa katiba ya Zanzibar," alisema.

Jussa aliwataka wananchi wa Zanzibar kumshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa fedha alizotenga kwa Zanzibar kusaidia sekta za kiuchumi kutetereka baada ya maradhi ya UVIKO-19 na kutoa mgawo wa fedha wa Sh. bilioni 230.

"Naomba mmpongeza kwa kumpigia makofi Rais Samia kwa fedha alizotenga kwa miradi ya maendeleo Zanzibar kufidia athari za UVIKO-19, haijawahi kutokea Zanzibar kupewa kiwango kikubwa cha fedha kama hicho," alisema Jussa.

Naye Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Othman Masoud, alisema fedha za umma siyo za mtu binafsi na matumizi yake yanapaswa kutumika kwa uwazi na kuzingatia maslahi ya wananchi.

Othman ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais, alisema ACT tayari imejipanga iwapo kitashika madaraka mwaka 2025 serikali yake haitofanya kazi kwa kificho kwa sababu ni kinyume na misingi ya utawala bora.

"Tukishika madaraka chama kitafanya kazi ya kusimamia serikali kulinda misingi ya utawala bora na siyo kuingia madarakani na kuanza kujifunza sisi tutakuwa kama askari wa miamvuli tukiruka, tukitua tunaendelea na kazi," alisema Othman.




Naibu Spika, Mussa Azzan 'zungu' (katikati), akiwa na baadhi ya wafanyakazi wa mgodi wa Barrick North Mara, walioshiriki mbio za City Marathon jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Dk. Mwinyi: Tanzania inatambua, kuheshimu usawa wa kijinsia

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema Tanzania inatambua na kuheshimu usawa wa kijinsia kwa kuona umuhimu wa kuwachagua wanawake kwenye mihimili yote ya nchi kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Aliyasema hayo, Ikulu, Zanzibar alipozungumza na uongozi wa taasisi ya kiraia, inayounganisha jumuiya za wanawake kutoka vyama mbalimbali vya siasa vyenye usajili nchini.

Miongoni mwa taasisi hizo ni Tasisi ya Sauti ya Wanawake wenye Ulemavu (SWAUTA), Chama cha Wabunge Wanawake (TWPG) na Umoja wa Wanawake wa Baraza la Wawakilishi (UWAWAZA) waliofika kumkabidhi tunzo kwa mafaniko aliyofanya katika uongozi wake.

Alisema serikali zote mbili zitaendelea kutoa fursa za kutosha kwa wanawake kwenye maeneo mbalimbali ili kutekeleza azma yao kufikia asilimia 50 kwa 50.

Alisema maendeleo yanataka usawa wa kijinsia kutoa haki na fursa sawa katika maendeelo ikiwamo elimu, afya na jamii kwa sababu kumwelimisha mwanamke kutaondoa changamoto nyingi kwenye jamii.

"Sijajuta hata kidogo kwa wale wanawake niliowateua kwenye serikali yangu, kwa kweli naona umuhimu wa kuwaongeza kwenye safu mbalimbali," alibainisha Rais Dk. Mwinyi.

Aidha, alisema serikali pia itaendelea kuimarisha huduma za mama na mtoto ili kupunguza changamoto nyingi kwa wanawake.

Rais Dk. Mwinyi aliwapongeza ULINGO kwa kazi kubwa wanayoifanya kuunganisha pamoja na kuwasifu kwa hatua yao ya kutanguliza maslahi mapana ya taifa, kuunganisha nguvu ya umoja wao bila kujali tofauti ya itikadi zao za kisiasa.

Alisema, Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania inatoa haki kwa jinsia zote kushiriki katika masuala ya siasa.

Viongozi wa taasisi hiyo pia walimpongeza Dk. Mwinyi kwa kutekeleza kwa vitendo masuala ya usawa wa kijinsia na ujumuishi wa makundi maalum katika ngazi za maamuzi, kulinda na kudumisha amani, umoja na utulivu nchini.

Pia walimpongeza Rais Dk. Mwinyi kwa kutambua kikwazo kinachowanyima fursa wanawake ikiwamo ukosefu wa elimu, matatizo kwenye sekta ya afya.

Makamu Mwenyekti wa taasisi hiyo Zanzibar ambaye ni Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mgeni Hassan, walimwahidi Dk. Mwinyi kwamba ifikapo mwaka 2025 atarejeshwa tena madarakani kwa nguvu na umoja wa wanawake.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**KELVIN RICHARD SAFARI,** Anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye Jina la **GS GROUP LTD** Namba za usajili **MC 259 DKH** aina ya **HAOJUE.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa Kituo cha Polisi.

TAARIFA YA POLISI:

**DOD/DOD/RB/123252/2023**

## KUPOTEA KWA CHETI CHA USAJILI

**SISTERS JOSEAN** WA MATEKA –SONGEA WANATANGAZA KUPOTEA KWA CHETI CHA USAJILI CHA **SISTERS OF SAINT JOSEPH OF CHAMBER** AMBACHO CHENYE NAMBA YA USAJILI **14027** KWA YEYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KATIKA KITUO CHA POLISI

KIMERIPOTIWA POLISI: **SOG/RB/2890/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HAMADI SHABANI ATHUMANI**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 463 CVC .** Chasses Namba **FK622M540005,** Engine Namba **6D16858990** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi . Polisi Taarifa : **KIL/MWA/RB/186754/2023**

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MASJALA NDOGO YA TEMEKE**
**(TEMEKE KITUO JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**
**MIRATHI NA 58 YA MWAKA 2023**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**JEHANGIR KERMALI BHALOO**
**NIGHAT JEHANGIR BHALOO..................MWOMBAJI**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 30 mwezi wa 06, 2023

**Imesainiwa Dar es salaam, leo tarehe 05 mwezi wa 06, 2023**

NAIBU MSAJILI

**3 FORM 58**
**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 615 OF 2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE DAVID NDENGERIO SWAI**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LATER OF ADMINISTRATION**
**BY MARK OMAR CHIGULU**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

**ALL PERSON** claiming to have any interest in the Estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 16th day of July, 2023.

**Dated at DAR ES SALAAM this 12th day of June, 2023.**

Senior Resident Magistrate

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**IRINGA**
**SHAURI LA RUFAA YA JINAI NA. 1 YA MWAKA 2023**
**THE DIRECTOR OF PUBLIC PROSECUTION (DPP)**
**MRUFANI**
**DHIDI YA**
**ADAM PATRICK MHAGAMA MJIBU RUFAA**

### KUITWA SHAURINI

**Kwa: ADAM PATRICK MHAGAMA,**
**POPOTE ULIPO.**

Shauri tajwa hapo juu limepangwa kutajwa tarehe 03.07.2023 saa tatu kamili (3:00) asubuhi. Hivyo kwa Mujibu ya maombi katika shauri hilo unatakiwa kufika katika Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Iringa kupitia Wakili wako au kutuma mwakilishi anayetambuliwa kisheria.

Fahamu kuwa endapo hutatuma mwakilishi wako, shauri hilo linaweza kusikilizwa upande mmoja bila wewe kuwepo.

**Imesainiwa hapa Iringa leo tarehe 01/06/2023.**

S. A. MKASIWA
KAIMU NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
KANDA YA IRINGA

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**PHILIPO ABRAHAM** LENGI ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 584 BWR** aina ya SKY GO. CHASSIS NAMBA **IFSGE2PK004189.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI.

TAARIFA YA POLISI:

**ARU/ARU/RB/200729/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PETER L. LINDSTUM**

anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 963 AHR** aina ya **PEUGEOT**. Chassis namba **4076615.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi.

Taarifa ya Polisi:

**ARU/ARU/RB/200328/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI**
**IDARA YA UHAMIAJI**

ANUANI YA SIMU:"UHAMIAJI"
TELEFAX: +255 28 280 2239
SIMU +255 28 280 2239/2391
E-MAIL:riokigoma@immigration.go.tz

OFISI YA WILAYA,
S.L.P 190,
KIGOMA.
16/05/2023



**Hii ni kuwaarifu kwamba MWENGE NGOY MUYOMBI**
Mwenye picha hapo juu anaomba Uraia wa Tanzania kwa Mh Waziri wa Mambo ya ndani ya Nchi, Utaifa wake wa sasa ni MKONGO, Nchi atokayo ni DRC, shughuli zake ni MKURUGENZI, mwenye pasipoti namba OP0302528 na kibali cha ukaazi namba RPH CO1818921AOO, kibali cha kazi namba 24240/21 mwenye namba ya simu 0752371818 na yupo hapa nchini tangia mwaka 1993.

Kwa yeyote mwenye sababu za kwanini mwombaji asipewe Uraia wa Tanzania, atume taarifa ya maandishi kwa Kamishna Jenerali wa Uhamiaji Tanzania,S.L.P NAMBA 1181 Dodoma Tanzania.

**K.n.y: KAMISHNA JENERALI WA UHAMIAJI TANZANIA**

**DEED POOLON CHANGE OF NAME**
**(Under the registration of Document Act (.1777 R: E OF 2002)**

By this deed I, LATIFA OTHMAN NG'OMBO of post office Box 328, Mtama,LINDI, a natural born Tanzanian citizen do hereby absolutely renounce and abandon the use of the former name of LATIFA ATHMAN MARKUS NG'OMBO in lieu thereof do assume and adopt the name of LATIFA OTHMAN NG'OMBO and in pursuance of such change of the name as aforesaid I,HEREBY DECLARE that I shall at all times thereafter in all records ,deed and instruments ,in writing and all actions and proceedings and in all dealings and transaction and upon all occasions whatsoever use and sign the said name of LATIFA OTHMAN NG'OMBO as my name in lieu of the said name of LATIFA ATHMAN NG'OMBO as aforesaid.I, HEREBY AUTHORISE AND REQUEST all person to designate and address me in the name of LATIFA OTHMAN NG'OMBO only.

IN WITNESS THEREOF I have hereunto subscribed my name of LATIFA OTHMAN NG'OMBO on the day and manner hereinafter appearing.SIGNED and DELIVERED by the saidLATIFA OTHMAN NG'OMBOWho is known to me personally /identifiedIn my presence this 30th day of May 2023BEFORE ME;
COMMISSIONER FOR OATHS DEPONENTDRAWN
BY;Adv.Mariam Kassim KashulweP.O.Box 2321,Morogoro

DEPONENT
BEFORE ME:
COMMISSIONER FOR OATHS
DRAWN BY:



**DEED POOLON CHANGE OF NAME**
**(Under the registration of Document Act .1777 R: E OF 2002)**

By this deed I, SOMOE MWALIMU NG'OMBO of post office Box 461,LINDI, a natural born Tanzanian citizen do hereby absolutely renounce and abandon the use of the former name of SOMOE MWALIMU M-BISI, in lieu thereof do assume and adopt the name of SOMOE MWALIMU NG'OMBO and in pursuance of such change of the name as aforesaid

I,HEREBY DECLARE that I shall at all times thereafter in all records ,deed and instruments ,in writing and all actions and proceedings and in all dealings and transaction and upon all occasions whatsoever use and sign the said name of SOMOE MWALIMU NG'OMBO as my name in lieu of the said name of SOMOE MWALIMU M-BISI, as aforesaid.

I, HEREBY AUTHORISE AND REQUEST all person to designate and address me in the name of SOMOE MWALIMU NG'OMBO only.

IN WITNESS THEREOF I have hereunto subscribed my name of SOMOE MWALIMU NG'OMBO on the day and manner hereinafter appearing.SIGNED and DELIVERED by the saidSOMOE MWALIMU NG'OMBO Who is known to me personally /identifiedIn my presence this 30th day of May 2023BEFORE ME;

COMMISSIONER FOR OATHS DEPONENTDRAWN
BY;Adv.Mariam Kassim KashulweP.O.Box 2321,Morogoro

DEPONENT
BEFORE ME:
COMMISSIONER FOR OATHS
DRAWN BY:



## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MARIA MBOTTO WANDIBA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili **T 886 CMU** aina ya **TOYOTA HARRIER.** Chassis namba **SXU150003311.** Chassis namba **5S0718208.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **ARU/ARU/RB/198899/2023**

**FORM NO. 58**
**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 48 OF 2023**

**In Matter of the Estate of the Late ERICK CRIZANTUS MGWESA**

**By 1. CHRIZANTUS MGWESA**
**2. ..................................**

All Persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or latter of administration) is made to the above - named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the **15TH JUNE 2023**

Dated at **Morogoro**, this **18TH** day of **MAY, 2023**

RESIDENT MAGISTRATE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo Wilaya ya MOROGORO**
**Kituo cha MJINI**
**Mkoa MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi Na. 53 /2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU GEORGE ABRAHAM wa BIGWA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA OMARY GEORGE**

### TANGAZO

**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe **23** Mwezi **06** mwaka **2023** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia:** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa

* Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
* Marehemu hakuacha wosia *Futa isiyohusika

Imetolewa leo tarehe **08** mwezi **06** mwaka **2023**

## KUPOTEA KWA CHETI



**YUSUPH A. LIGWEMA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S1659-0304 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ABOUD JUMBE SECONDARY SCHOOL** mwaka **2016.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: MOR/MOR/RB/198484/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya SINGIDA**
**Kituo cha MJINI Mkoa SINGIDA**
**Shauri la Madai Na. 11/2023**
**JINA LA MDAI...................ATHUMANI RASHIDI ALLY**
**JINA LA MDAIWA............RONNY MUGAMBI**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za utaratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**KWA: RONNY MUGAMBI**
**Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba**
**MADAI YA TSH. 8,000,000/=**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 14/06/2023 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujjitetea.

ANGALIZO kama hautohudhuria siku ilitajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 08/06/2023.

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
MJINI-SINGIDA

**IN THE DISTRICT COURT OF KONGWA DISTRICT**
**AT KONGWA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.02 OF 2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE GODFREY TITO MAUMBI**
**DESEASED OF KONGWA - DODOMA**
**AND**
**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY**
**ROBART GODFREY MAUMBI............. PETITIONER**
**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN NO.369 OF 1963)**

All persons claiming to have any interest in the Estate of the above - named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of Administration) is made to the above - named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 09th day of JUNE, 2023.

The will of the said deceased is deposited and open for inspiration at the Court.

**Date 23RD day of MAY, 2023**

District Resident Magistrate

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



Mkurugenzi wa TEHAMA wa Kampuni ya Vodacom Tanzania, Athumani Mlinga (wa tatu kulia), akimwangalia mwanafunzi wa shule ya kituo cha kulelea watoto yatima cha Kiwalani, Janeth Lwanga, aliposoma mojawapo ya kitabu, baada ya kampuni hiyo kutoa msaada wa vifaa mbalimbali ikiwamo madawati, meza, viti, vitanda, magodoro, na kompyuta vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 21 kwa niaba ya wafanyakazi wa Vodacom mwishoni mwa wiki. Wengine ni Mwenyekiti wa CCM Kata ya Kiwalani, Leornard Msusu (kulia), Ofisa Mtendaji wa Kata hiyo, Lucresia Shayo (wa pili kulia) na Mwalimu wa kituo hicho, Yustina Myovera (nyuma ya mwanafunzi). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Rushwa ya ngono kikwazo wanawake kushiriki ununuzi

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

USHIRIKI wa wanawake katika ununuzi wa umma umebainika kuwa chini nchini kutokana na kuchangiwa na masuala mbalimbali ikiwamo rushwa ya ngono.

Hayo yamo katika ripoti ya utafiti wa ushiriki wa wanawake katika ununuzi wa umma uliofanywa na Kituo cha Africa Freedom of Information Centre (AFIC) katika nchi tano za Kenya, Uganda, Ethiopia, Rwanda na Tanzania.

Akiwakilisha matokeo ya utafiti huo kwa waandishi wa habari jana jijini hapa, Mkurugenzi Mkuu wa AFIC, Gilbert Sendugwa alisema hali hiyo pia inachangiwa na uelewa mdogo, lugha ngumu na ya kitaalamu inayotumika katika mikataba ya ununuzi wa umma, sera ngumu na mfumo dume unawanyima fursa wanawake kushiriki katika sekta hiyo muhimu.

Alisema utafiti huo umebaini wanawake wengi hawana taarifa, wala hawajui namna ya kuomba zabuni mbalimbali za ununuzi wa umma.

"Takribani asilimia 60 ya ununuzi wa nchi unatumika katika sekta ya ununuzi wa umma, hivyo ni jambo la kizalendo kuhakikisha nchi inaweka mazingira na sera nzuri ya kuhakikisha wanawake wananufaika na matunda ya ukuaji wa uchumi wa nchi yao," alisema.

Aliongeza kuwa utafiti unaonyesha asilimia 48 ya biashara zote nchini zinamilikiwa na wanawake, lakini jambo la kusikitisha ni namna ambavyo wanawake hao wametengwa katika fursa za kunufaika na kandarasi mbalimbali zinazojitokeza katika sekta ya ununuzi wa umma.

"Kwa mfano, Sheria ya Ununuzi wa Umma inaelekeza kwamba ili kupata nafasi ya kuhudumia mkataba wa ununuzi wa umma, walengwa lazima wawe katika kikundi na siyo mtu binafsi, hatua hii inawanyima haki ya msingi wanawake wenye kampuni yao binafsi kunufaika," alisema.

Mratibu wa Ufuatiliaji na Tathmini wa AFIC, Charity Komujjurizi, alisema kuna umuhimu wa wizara husika kushirikiana na wadau wengine wa sekta ya ununuzi wa umma katika kuwaelimisha wanawake namna bora ya kuomba na kunufaika na fursa mbalimbali zinazojitokeza katika ununuzi wa umma nchini.

"Kwa mfano, Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA) huwa wanatoa tenda za ununuzi wa umma katika huduma muhimu, hivyo ni muhimu wawe wanatoa kipaumbele kwa wanawake wajasiriamali katika maeneo husika," alishauri.

Akipokea matokeo ya utafiti huo, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii na Maendeleo ya Jamii, Fatma Toufiq, alipongeza AFIC kwa kufanya utafiti huo muhimu. Kamati itaishauri serikali kuyafanyia kazi mapendekezo mbalimbali yaliyoainishwa katika ripoti hiyo.

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## MAOMBI YA KUONESHA NIA YA UTOAJI WA HUDUMA YA KUTATHMINI NA KUCHAGUA WATAHINIWA WALIOFUZU HATUA YA MOOC NCHINI TANZANIA KUMBUKUMBU NA. 0000000206

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) Ltd, ambayo ni Kampuni ya mafuta na gesi, inaalika kampuni au taasisi yenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya kutoa huduma ya kutathmini na kuchagua watahiniwa waliofuzu hatua ya MOOC nchini Tanzania katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili kwa ajili ya kusafirisha mafuta ghafi kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka mashariki mwa pwani ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa waTanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU HUDUMA:**
Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) Ltd imeanzisha jukwaa kubwa la Kozi Huria kwa Njia ya Mtandao (Massive Open Online Course - MOOC) ikiwa ni mojawapo ya dhamira yake katika kukuza watoa huduma wa ndani na ushiriki wa raia wa Tanzania katika mnyororo wa thamani wa Mafuta na Gesi, ambapo watahiniwa watahitimu kozi kadhaa kama sehemu ya mchakato wa mchujo wa kupata watahiniwa bora. Mchakato huo utafuatiwa na usahili utakaofanywa na EACOP kwa kushirikiana na mtoa huduma ya uajiri wa nje ya EACOP.

Hivyo basi, Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) Ltd, inatafuta mtoa huduma wa nje ili kusaidia kufanya tathmini na kuchagua watahiniwa kwa ajili ya programu hii kulingana na shughuli zilizotajwa hapo chini:

**Ukaguzi wa ustahiki wa watahiniwa.**
- Kuchuja ustahiki wa watahiniwa (kwa vigezo kama vile; utaifa, umri, n.k).
- Kufanya tathmini za kiufundi (kwa mahojiano au maandishi)
- Kuendesha mitihani au majaribio ya kupima vipaji na uwezo wa kiakili
- Uhakiki wa sifa za kitaaluma za watahiniwa
- Kufanya ukaguzi wa usuli/rejea za tabia

**Mchakato wa usahili**
- Kuwasiliana na watahiniwa.
- Kuwasimamia watahiniwa katika mchakato wa usahili
- Kuandaa majaribio ya papo kwa papo ili kuhakiki matokeo ya MOOC ya EACOP
- Kupanga ratiba ya usahili wa ana kwa ana
- Kushika/kuandaa mahali pakufanyia usahili
- Kuwasilisha ripoti ya kuajiri ya mchakato mzima wa kuajiri katika kila hatua
- Kuwapatia mrejesho na taarifa watahiniwa wanaofanyiwa tathmini na kuchaguliwa

**Wakati mtoa huduma wa nje atakapokuwa anatekeleza majukumu yake anapaswa:**
- Kuonyesha viwango vya juu zaidi vya utaalamu na kutumia uangalifu, ujuzi na umahiri unaostahili ili kutoa huduma kulingana na mahitaji ya EACOP.
- Kwa kuzingatia sera zote husika za EACOP na utendaji bora wa kimataifa pamoja na sheria husika za nchi, ikiwa ni pamoja na sheria za nchi zinazohusu ubaguzi (ubaguzi wa kijinsia au kikabila).
- Kuandaa na kukabidhi ripoti zote muhimu.

**VIGEZO MUHIMU:**
**Makampuni au taasisi zinazoonesha nia zinaalikwa kutuma maombi kwa kuambatanisha nyaraka zifuatazo:**
- Uthibitisho wa usajili kutoka mamlaka husika ikiwa ni pamoja na Leseni ya Biashara
- Uthibitisho wa uzoefu wa kutoa huduma zinazofanana na hii au kampuni ikiwa ni pamoja na barua ya uthibitisho kutoka kwa wateja watatu wa hivi karibuni.
- Wafanyakazi waliopendekezwa wenye sifa na uzoefu
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na cheti cha uthibitisho wa mlipa kodi kwa mwaka wa fedha hivi karibuni.
- Uthibitisho wa usajili au maombi ya kujisajili yaliyothibitishwa kwenye kanzi data ya EWURA ya Watoa Huduma ya Ugavi wa Ndani (LSSP) wakati wa kuonesha nia.
- Kukidhi Kanuni za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017 na fasili ya Kampuni ya Ndani.
- Uthibitisho wa kukubaliana na sera za kupinga rushwa, ufisadi, na Haki za Binandamu

Kampuni zenye nia, ambazo zina uwezo na rasilimali za kutosha kutoa huduma zilizotajwa hapo juu zinapaswa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi **20Mb**) kabla ya tarehe **27/06/2023** saa 11:00 jioni kwa Saa za Afrika Mashariki (EAT). Kichwa cha Barua pepe kiwe 0000000206 (**kumbukumbu namba iliyoonyeshwa hapo juu ya barua**). Maombi yote yakuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20. Maombi yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiingereza.

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya makampuni ya awali yenye vigezo. Mwaliko wa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa makampuni ya awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wataarifa (NDA).

# JOB: TUZO IMENIPA DENI MSIMU UJAO

**Na Shufaa Lyimo**

BEKI wa klabu ya Yanga, Dickson Job ambaye usiku wa kuamkia jana alichaguliwa kuwa beki bora wa Ligi Kuu msimu wa 2022/2023 amesema tunzo hiyo aliyoipata itakuwa chachu ya kujituma na kupambana zaidi msimu ujao na kuonyesha hakupata kwa bahati mbaya.

Akizungumza baada ya kupokea tunzo hiyo alisema msimu ulikuwa mgumu na wenye ushindani mkubwa lakini anashukuru kwa kupata tuzo hiyo yenye maana kubwa kwake na imempa deni la kuhakikisha anafanya vizuri zaidi msimu ujao.

"Tunzo hii imeniongezea chachu ya kuongeza ushindani msimu ujao nikishirikiana na wachezaji wenzangu, kuna mabeki wengi sana wazuri lakini hii kwangu imekuwa zaidi ya zawadi, itanifanya nijitume zaidi msimu ujao," alisema Job.

**Alisema anaushukuru uongozi wa klabu hiyo, wachezaji pamoja na benchi la ufundi kutokana na ushirikiano walioompa muda wote wa msimu ambao wamefanikiwa kutwaa ubingwa wa ligi na kombe la FA.**

"Lakini nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipomshukuru meneja wangu George Job, amekuwa msaada mkubwa kwangu na yeye ni sehemu ya mafanikio haya niliyoyapata msimu huu," alisema Job.

Alisema kipindi hiki ambacho timu zote zinaelekea mapumziko atakitumia kufanya mazoezi binafsi kwa lengo la kuboresha kiwango chake.

Wakati huo huo Clement Mzize ambaye alipata tunzo ya mchezaji bora mwenye umri chini ya miaka 20 (U-20) alisema tunzo aliyoipata imemfanya awake historia kwenye maisha yake ya mpira.

"Tunzo hii ni muhimu kwangu ukiangalia vijana wenye umri kama wangu walikuwa wengi isipokuwa kamati imeona mimi nina vigezo vya kuibeba," alisema Mzize.

Alisema siri ya mafanikio yake ni kujituma na kufuata maelekezo ya kocha wake na kutoa ushirikiano kwa wachezaji wenzake.



# Balozi Mkingule aitabiria neema Twiga Stars 2023

**Na Mwandishi Wetu,** LUSAKA

LICHA ya kupoteza mechi ya kirafiki ya kimataifa, Balozi wa Tanzania nchini Zambia, Luteni Jenerali Mathew Mkingule, amesema Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), ilionyesha kiwango kikubwa katika mchezo huo na kuwapa 'joto' wenyeji (Copper Queens).

Twiga Stars ilifungwa bao 1-0 na Copper Queens katika mechi ya kirafiki ya kimataifa iliyochezwa Jumapili iliyopita kwenye Uwanja wa Woodlands jijini hapo.

Akizungumza katika chakula cha jioni alichowaandalia juzi usiku, Balozi Mkingule, alisema kwa ushindani walioonyesha Twiga Stars, anaamini itapata matokeo mazuri katika kampeni zake za kusaka tiketi ya kushiriki mashindano mbalimbali ya kimataifa.

Mkingule alisema amefurahishwa na juhudi za kila mchezaji wa timu hiyo na amewataka kuendeleza nidhamu ili wafikie malengo yao kama timu na kuipa heshima Tanzania.

"Nawapongeza sana kwa namna mlivyocheza vizuri mechi ile, mliwapa hofu sana, hawakuamini namna mlivyowabana, ilifika wakati wakawa wanaomba mechi imalizike kwa sare wakati kabla ya kuanza waliamini itakuwa nyepesi kwao," alisema Mkingule.

Aliwatakia safari nje ya kurejea nyumbani na kuahidi kuendelea kutoa ushirikiano na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) katika maandalizi ya timu wakati wowote watakapokwenda Zambia kushindana.




Msanii wa Hiphop, Kontawa, akitoa burudani kwa wanafunzi wa vyuo vikuu jijini Mbeya katika Tamasha la 'Boomplay TECNO Campus Tour' lililofanyika Chuo cha Uhasibu (TIA) jijini humo mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Tabora United kufanya usajili wa nguvu Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Kitayosce iliyopanda daraja msimu huu na kubadilisha jina na kuwa Tabora United, imesema itasajili wachezaji wenye viwango vya kucheza Ligi Kuu Tanzania msimu ujao.

Msemaji wa klabu hiyo, Pendo Lema amesema baada ya kupanda Ligi Kuu, benchi la ufundi limefichua kuwa kuna mapungufu baadhi ya maeneo ambapo inatarajia kuongeza wachezaji wenye uwezo mkubwa.

"Tumefanikiwa kupanda Ligi Kuu, ni furaha kwa Wanatabora wote, tunajua kuwa pamoja na kupanda Ligi Kuu, kuna mapungufu ambayo benchi la ufundi imeyabaini, siwezi kusema tunasajili wachezaji wa aina gani na kutoka wapi, lakini viongozi wetu wapo makini na wanalifanyia kazi hilo, tunajua ugumu wa Ligi Kuu lakini hata huku tulipotoka ni kugumu pia tuna uhakika kuwa tutapata wachezaji wenye viwango vya huku tuliko sasa," alisema Lema.

Pamoja na kusaka wachezaji wengine, lakini timu hiyo ina baadhi ya wachezaji kutoka nje ya nchi, wakiongozwa na straika wao hatari aliyechangia timu hiyo kuwa hapo ilipo, Mkongomani Fabrice Ngoy wa Ngoy aliyeshika nafasi ya pili kwenye nafasi ya ufungaji bora, akiwa na mabao 15 akizidiwa Edward Songo wa JKT Tanzania ambaye alitwaa tuzo ya uchezaji bora wa ligi ya daraja la kwanza msimu huu.

# Boomplay, Tecno wahitimisha tamasha wanavyuo

**Na Mwandishi Wetu**

BOOMPLAY kwa kushirikiana na Kampuni ya Tecno Mobile Tanzania juzi walihitimisha kwa mafanikio ziara yao ya kutembelea vyuo mbalimbali mkoani Mbeya kwa kufanya tamasha kubwa la muziki kwenye viwanja vya Chuo cha Uhasibu jijini hapo.

Ziara hiyo ya Kanda ya Kusini ililenga kusherehekea ushirikiano mzuri wa teknolojia na muziki ambapo elimu mbalimbali juu ya teknolojia ilitolewa kwa wanafunzi wa vyuo vya mkoani hapa.

Ziara hiyo ya vyuo imedumu kwa wiki nne, ikijumuisha vyuo vikuu vinne vya mkoani hapa ambavyo ni Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA), Chuo cha Mzumbe, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE).

Akizungumza jijini hapo, Meneja Mkuu wa Boomplay Tanzania, Natasha Stambuli, alisema ziara hiyo imeonyesha namna muziki ulivyo na nguvu ya kuwakutanisha watu pamoja na kujenga ushirikiano.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RICE AKARIBIA ARSENAL

ARSENAL inakaribia kufikia makubaliano ya pauni milioni 100 kumsajili kiungo wa kati wa West Ham na England, Declan Rice, 24. ***(Guardian)***

### GUARDIOLA KUONDOKA

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola anapanga kuondoka katika klabu hiyo mkataba wake utakapokamilika mwaka 2025. ***(Guardian)***

### GVARDIOL BEI JUU

KLABU ya RB Leipzig itahitaji ada ya angalau pauni milioni 75 ikiwa inataka kumuuza mlinzi wa Croatia, Josko Gvardiol, 21, kwa Manchester City. ***(Sport)***

### MAN CITY ILIKATAA

KLABU ya Manchester City ilikataa ofa ya Paris St-Germain ya kuwajumuisha kiungo wa kati wa Italia, Marco Verratti, 30 na kipa wa Italia, Gianluigi Donnarumma, 24, kama sehemu ya makubaliano ya kumsajili mchezaji wa Ureno, Bernardo Silva kutoka kwa washindi hao wa mataji matatu msimu huu. ***(Footmercato)***

### CHELSEA YAHOFIA

ARSENAL inahofia Chelsea inaweza kuwashinda katika kumsajili kiungo wa kati wa Brighton, Moises Caicedo, 24, kwa kumpa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ecuador fedha zaidi. ***(football Transfers)***

### ONANA ALENGWA

CHELSEA imemfanya mchezaji wa kimataifa wa Cameroon, Andre Onana, 27, kuwa wanayemlenga sana huku wakitafuta mlinda mlango mpya na Inter Milan wanataka angalau pauni milioni 50 kwa mchezaji huyo. ***(Evening Standard)***

### MAN YAKOMAA NA MOUNT

KLABU ya Manchester United inaendelea na mazungumzo na Chelsea kuhusu kiungo wa kati wa England, Mason Mount, 24, lakini bado kuna pengo la tathmini kati ya klabu hizo mbili kwa mchezaji huyo. ***(Sky Sports)***

### HARRY KANE HAUZWI

KLABU ya Manchester United haina uwezekano wa kumnunua mshambuliaji wa Tottenham, Harry Kane, 29, kwani Spurs hawataki kumuuza nahodha huyo wa England, haswa kwa timu nyingine ya Ligi Kuu. ***(Sky Sports)***

### RAYA AWINDWA

TOTTENHAM Hotspur inatazamiwa kuwasiliana na Brentford ili kujadili kuhusu ada ya kumnunua kipa wa Hispania, David Raya, 27. Lakini Spurs na wawindaji wenzao Manchester United wanasita kulipa pauni milioni 40 ambazo zinatakiwa kwa mchezaji huyo. ***(Sky Sports)***

### ZAHA KWENDA SAUDIA

WINGA wa Crystal Palace, Wilfried Zaha, 30, anatazamiwa kukataa ofa ya pauni milioni 30 kwa mwaka ili kujiunga na klabu ya Saudi Arabia Al-Nassr, huku Paris St-Germain na Marseille zikiwa na nia ya kumsajili mshambuliaji huyo wa Ivory Coast kwa uhamisho wa bila malipo msimu huu. ***(Guardia)***

## DONDOO SOKA MAGAZETI ULAYA




# MBAPPE RASMI SOKONI

**PARIS,** Ufaransa

KLABU ya Paris St-Germain iko tayari kumuuza Kylian Mbappe msimu huu wa joto kwa hofu ya kumpoteza kama mchezaji huru mara mkataba wake utakapomalizika mwakani, baada ya kuiambia klabu hiyo ya Ufaransa kuwa hataongeza mkataba wake.

**Mkataba wa sasa wa mchezaji huyo wa Ufaransa unamalizika mwishoni mwa msimu ujao, kukiwa na chaguo la kuongeza mwaka mwingine.**

Huku PSG wakiwa hawataki Mbappe aondoke kama mchezaji huru baada ya msimu ujao, duru zilisema mwenyekiti wa klabu hiyo, Nasser Al Khelaifi sasa yuko wazi kumruhusu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 kuondoka jijini Paris.

Vyanzo vya ESPN viliongeza kuwa PSG itataka ada itakayofikia euro milioni 150 ili kumwachia.

Mwaka jana, PSG ilikataa dau la euro milioni 180 kutoka kwa Real Madrid, ambao walikuwa wanamtaka Mbappe tangu akiwa na umri wa miaka 11.

Mshambuliaji huyo huenda akahusishwa tena na kuhamia Madrid, hasa baada ya Karim Benzema kuwaacha wababe hao wa LaLiga na kujiunga na timu ya Al-Ittihad ya Saudi Arabia.

**Mtazamo mpya ungekuwa kwa vijana na alitarajiwa kuwa kiini cha...**

Madrid tayari wamekubali kumnunua kiungo wa kati wa England, Jude Bellingham na uwezekano wa kumpata Mbappe utakuwa kauli ya dhamira kuu baada ya kuachia mataji yao ya LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu.

Mbappe alikuwa amekataa kuzungumzia mustakabali wake na PSG kufuatia kutolewa kwenye hatua ya 16 bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na Bayern Munich, Machi.

PSG, ambayo inamilikiwa na Qatar Sports Investments, tayari imemuona Lionel Messi akiondoka bila malipo, huku nyota huyo wa Argentina akihamia timu inayoshiriki Ligi Kuu ya Marekani, MLS, Inter Miami.

Pia kuna sintofahamu kuhusu mustakabali wa nyota mwingine wa PSG raia wa Brazil, Neymar.

Lakini uwezekano wa kuondoka kwa Mbappe mwenye umri wa miaka 24 itakuwa hasara kubwa zaidi kwa PSG, ikizingatiwa kwamba yeye ni nyota anayechukuliwa kuwa mmoja wa wachezaji wachache wenye uwezo wa kuchukua mikoba ya Messi na Cristiano Ronaldo kama nyota mkubwa zaidi wa mchezo huo duniani.

Mbappe alikuwa na hadi Julai 31 kuanzisha mazungumzo ya kuongeza mkataba wa mwaka mmoja.

Amekuwa katika klabu hiyo tangu mwaka 2017 baada ya kusajiliwa kutoka AS Monaco kwa uhamisho wa thamani ya dola milioni 190.

PSG walikuwa wakipanga mabadiliko ya mkakati baada ya uhamisho wa nyota hao wakubwa kushindwa kuleta mafanikio Ulaya.

Mtazamo mpya ungekuwa kwa vijana na Mbappe alitarajiwa kuwa kiini cha mabadiliko hayo na ilitarajiwa angesaini mkataba wa muda mrefu zaidi.

Mbappe ameshinda mataji matano ya ligi ya Ufaransa akiwa na PSG na alikuwa mshindi wa Kombe la Dunia akiwa na Ufaransa mwaka 2018.

Ana mabao 38 katika mechi 68 alizoichezea Ufaransa, ikiwa ni pamoja na mabao matatu kwa mpigo katika fainali ya mwaka jana nchini Qatar, Ufaransa ilipofungwa na Argentina kwa mikwaju ya penalti.

Mbappe alimaliza kama mfungaji bora wa Ligue 1 katika kila misimu mitano iliyopita.

PSG ilimaliza msimu wa 2022-23 kwa kutwaa taji la Ligue 1 pekee baada ya kushindwa tena kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.



# GUARDIOLA ANAFIKIRIA KUONDOKA MAN CITY

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola hatarajii kusaini mkataba mpya na Manchester City mara huu wa sasa utakapomalizika mwaka 2025, kwa mujibu wa ESPN.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, Guardiola mwenye umri wa miaka 52 bado hajafanya uamuzi kuhusu mustakabali wake, lakini anaelekea kumaliza muda wake wa kukaa pale kwenye dimba la Etihad baada ya misimu miwili zaidi.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba Guardiola anaweza kutafuta kazi ya timu ya taifa, baada ya kuwaniwa na Brazil na Merika hapo awali.

Guardiola alisaini mkataba mpya na City Novemba, baada ya kusafiri hadi Abu Dhabi wakati wa mapumziko ya Kombe la Dunia.

Kocha huyo wa zamani wa Barcelona na Bayern Munich amepuuzilia mbali mapendekezo ya kwamba anaweza kuondoka msimu huu wa joto baada ya kukamilisha mataji matatu na kuwahakikishia mashabiki wa City Mei kwamba atakuwa kocha mwanzoni mwa msimu ujao.

Lakini vyanzo viliiambia ESPN kwamba tayari amekaa kwenye klabu kwa muda mrefu kuliko vile alivyofikiria wakati alipochukua nafasi hiyo mwaka 2016 na ana shaka ikiwa atatakaa kujadili mkataba mpya msimu ujao wa joto.

Msimu ujao utakuwa wa nane kuinoa City, alitumia miaka minne kuinoa Barcelona na miaka mitatu kama kocha wa Bayern.

Kwa mujibu wa ripoti City haijakata tamaa kwamba Guardiola anaweza kuamua kusalia zaidi, lakini wataheshimu uamuzi wake ikiwa anataka kuondoka.




# *Vinicius Junior apewa jezi namba 7*

**MADRID,** Hispania

MCHEZAJI Vinícius Júnior sasa atavaa jezi nambari 7 ya Real Madrid -- iliyokuwa ikivaliwa na Cristiano Ronaldo -- msimu ujao baada ya kuondoka kwa Eden Hazard, klabu hiyo imethibitisha.

Vinicius mwenye umri wa miaka 22 kwa sasa ameorodheshwa kama namba 7 wa Madrid katika sehemu ya kikosi cha kwanza cha tovuti ya klabu hiyo.

Aidha, mchezaji mwenzake wa kimataifa wa Brazil, Rodrygo Goes atavaa namba 11, baada ya Marco Asensio kuondoka klabuni hapo. Vinicius alivaa jezi nambari 20 msimu uliopita, huku Rodrygo akivaa namba 21.

Wachezaji hao wawili sasa ni viungo muhimu kwenye kikosi cha kwanza, wakifunga mabao 19 ya LaLiga na 12 ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita.

Hazard alivaa namba 7 ya Madrid tangu alipowasili Santiago Bernabeu Julai 2019 hadi kuondoka kwake mwezi huu.

Mbelgiji huyo alikubali kufikia makubaliano ya kusitisha mkataba wake ambao ulibakiwa na mwaka mmoja, baada ya miaka minne ya kukatisha tamaa nchini Hispania.

Ronaldo alivaa namba 7 kwa misimu nane kati ya 2009 na 2018, na kuwa mfungaji bora wa muda wote wa Madrid akiwa na mabao 450, na kushinda mataji manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Wachezaji wa zamani wakubwa wa Real Madrid waliwahi kuvaa namba 7 ni Raul Gonzalez, ambaye kwa sasa anafundisha timu ya akiba ya klabu hiyo, Emilio Butragueño, ambaye ni mkurugenzi wa uhusiano wa kitaasisi wa Madrid, Amancio Amaro, ambaye alikuwa rais wa heshima wa Madrid hadi kifo chake Februari na Juan "Juanito" Gomez.

## Neymar: Messi atabadilisha soka Marekani

**NEW YORK,** Marekani

NEYMAR amesema kuhamia kwa Lionel Messi katika Klabu ya Inter Miami kutaubadilisha mchezo wa wa Ligi Kuu ya soka ya Marekani.

Wiki iliyopita, Messi alitangaza uamuzi wake wa kujiunga na Inter Miami mara tu mkataba wake na Paris Saint-Germain utakapomalizika mwishoni mwa mwezi huu.

"Nina uhakika kwamba Leo atabadilisha ligi nchini Marekani," alisema Neymar.

"Ninaamini ligi itakuwa maarufu zaidi. Kwa hiyo kila mmoja anapaswa kutumia fursa na kufurahia kumtazama akicheza kwa sababu kwa bahati mbaya hakuna kinachodumu milele."

Messi alikuwa na ofa za kurejea klabu ya zamani ya Barcelona na angeweza kuhamia klabu ya Al Hilal ya Saudi Arabia, lakini hatimaye aliamua kujiunga na Inter Miami -- timu ambayo mmoja wa wamiliki wake ni David Beckham.

Neymar, ambaye alicheza na Messi kule Barca na PSG, amechanganya hisia kuhusu uamuzi wa Messi, ambao anaouona kuwa usajili mkubwa zaidi katika historia ya miaka 27 ya soka la Marekani.

"Nina huzuni na furaha kwa wakati mmoja," alisema fowadi huyo wa Brazil.

"Nilijua tayari. Messi ni mmoja wa marafiki zangu wa karibu, zawadi ambayo soka imenipa. Nilipata fursa ya kumfahamu, kucheza naye na kisha kujenga urafiki mzuri.

"Kwa hiyo, nilijua kwamba angeweza kuja hapa (Miami), na tulizungumza kuhusu hilo. Nilimwambia angefurahi sana jijini, kwa sababu ya mtindo wa maisha, fursa ya kuja kuishi na kucheza hapa Miami."

Neymar amekuwa akiishabikia Miami Heat wakati wa Fainali za mpira wa kikapu wa Marekani, NBA.

Siku ya Ijumaa, alikuwa kwenye umati wa watu katika Kituo cha Kaseya na aliandamana na mchezaji mwenzake wa Brazil na mshambuliaji wa Real Madrid, Vinicius Junior wakati Heat ilipopambana na Denver Nuggets katika mchezo wa nne.



## Yanga yatoa msimamo wake, Mayele, Nabi

INATOKA UKURASA 24

Alisema mafanikio waliyoyapata msimu huu kuanzia michuano ya ndani na ya Kimataifa ndio imesababisha wachezaji na makocha wao kuhusishwa zaidi na timu nyingine nje ya Tanzania.

"Si rahisi kwa uongozi kuwaachia wafanyakazi wengi hao kuondoka, tutahakikisha tunabaki nao kwa sababu bado tunataka mafanikio zaidi msimu ujao," alisema na kuongeza,

"Si makocha tu ambao wamemaliza mikataba yao bali hata wachezaji na baadhi ya wafanyakazi wetu wengine ambao wako kwenye benchi la ufundi, hii ni hali ya kawaida tutakaa nao wale wote mikataba inayoisha na tutawaongezea," alisema.

Hata hivyo Hersi alisema kama itatokea watashindwana na mfanyakazi yeyote watamwachia bila kuwa na kinyongo naye chochote.

"Nasisitiza tutazungumza nao kama tutakubaliana watabaki ikitokea kama tutashindwa kuafikiana basi hatutakuwa na kinyongo kumruhusu mtu kuondoka kwenda sehemu nyingi kwa ajili ya kupata changamoto zingine na marisho bora zaidi," alisema Hersi.

**WAITEKA DAR KWA MAPOKEZI**

Katika hatua nyingine mashabiki wa Yanga jana walifurika kwenye mitaa ya Dar es Salaam kuipokea timu hiyo iliyotokea Tanga baada ya kutwaa ubingwa wa Kombe la Shirikisho (FA) kwa kuifunga Azam bao 1-0 kwenye mchezo wa fainali iliyochezwa Uwanja wa Mkwakwani.

Kikosi cha Yanga kiliwasili kwenye Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere majira ya saa 4:00 asubuhi na kuanza safari kuelekea Karume walipoanzia msafara wao huo maalum kuelekea makao makuu ya timu hiyo wakipitia barabara ya Msimbazi.

Basi maalum la Yanga ambalo lilikuwa linawasubiri wachezaji Karume lilianza msafara majira ya saa 5:00 likiwa limebeba wachezaji viongozi pamoja na makombe yao yote waliyoyapata msimu huu ambayo ni Kombe la Ligi Kuu, Kombe la Shirikisho (FA) na Ngao ya Jamii walioipata mwanzoni mwa msimu huu.

Mashabiki wengi walijitokeza na kujazana kwenye barabara ya Karume kuanzia saa 12 asubuhi kwa lengo la kuisubiria timu yao.

Msafara huo ulifika mitaa ya Jangwani majira ya saa saba mchana ambapo burudani mbalimbali zilikuwa zinaendelea klabuni hapo huku mashabiki wakiwa wamejazana kwenye viwanja hivyo.

Baada ya kuwasili moja kwa moja wazee wa Yanga walisoma dua kwa ajili ya kuiombea timu yao na kushukuru kwa kufanya vizuri msimu huu.

Msanii Diamond Platinum aliongoza wasanii wengine kwa kutoa burudani ya aina yake kwa saa mbili mfululizo mbele ya maelfu ya mashabiki waliojitokeza kuipokea timu hiyo.

Mbali na burudani hiyo, mashabiki wa klabu hiyo walilipuka kwa shangwe baada ya rais wa klabu hiyo, Hersi kumvalisha jezi ya Yanga Diamond na kutangaza kuhamia timu hiyo.

Ikumbukwe misimu miwili iliyopita, Diamond alihusishwa kuwa shabiki wa Simba baada ya kutunga nyimbo maalum ya ikisifia klabu hiyo pamoja na kutoa burudani kwenye kilele cha tamasha la Simba 'Simba Day'.

# SAIDO ATOA TUZO ZAKE KWA BOSI 'TRY AGAIN'

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji wa Simba, Saido Ntibazonkiza, amesema tuzo alizozipata usiku wa kuamkia jana anazitoa kwa Mwenyekiti wa bosi ya klabu hiyo, Salim Abdallah 'Try Again' ambaye alipambana kuhakikisha anacheza kwenye klabu hiyo.

**Saido alisema Try Again alimwamini na alihakikisha anasajiliwa na Simba na kucheza kwenye ligi msimu huu uliomalizika hivi karibuni.**

Aidha, alisema mbali na Try Again, tuzo hiyo pia anaitoa kwa wanachama na mashabiki wa klabu hiyo ambao walimpokea na kumpa sapoti kubwa na kumfanya kujituma na kupambana kwa ajili ya timu.

Saido juzi alipata tuzo nne ya kiungo bora, mchezo wa kiungwana 'fair play', kikosi bora cha msimu pamoja na tuzo ya mfungaji bora ambayo waligawana na mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele baada ya kulingana idadi ya mabao (17).

"Try Again, alinipambania sana ili niichezee klabu hii, alisikia maneno mengi, lakini alinikubali, akaniamini, akanipa nafasi, nadhani mwenyewe ananitazama na anafurahi kuona nimechukua hii tuzo," alisema Ntibanzonkiza muda mfupi baada ya kukabidhiwa tuzo hizo.

Ntibazonkiza na Mayele walifunika kwenye tuzo za Shirikishisho la Mpira wa Miguu (TFF) msimu wa 2022/23, wakichukua tuzo nyingi zaidi ya wenzao, kila mmoja akichukua tuzo nne katika hafla iliyofanyika Kituo cha Michezo, Mnyanjani jijini Tanga.

Mayele alipata tuzo ya Mchezaji bora wa mwaka (MVP), tuzo ya bao bora, kikosi bora cha msimu pamoja na tuzo ya bao bora ambayo aligawana na Ntibazonkiza.

Wengine walitwaa tuzo ni pamoja na golikipa wa Yanga, Djigui Diarra raia wa Mali, Dickson Job wa Yanga alichaguliwa kuwa beki bora wa mwaka, Lameck Lawi wa Coastal Union, alitwaa tuzo ya mchezaji bora chipukizi msimu huu na KMC imekuwa ni timu yenye nidhamu.

Kikosi bora cha wachezaji 11 msimu 2022/23 kimetajwa kuwa ni Diarra (Yanga) mabeki wa pembeni, Shomari Kapombe na Mohamed Hussein 'Tshabalala (Simba), Job na Bakari Mwanyeto (Yanga) na Henock Inonga wa Simba.

Viungo ni Mzamiru Yassin (Simba), Bruno Gomes (Singida Big Stars), Clatous Chama, Ntibanzokiza (Simba) na Mshambuliaji Mayele (Yanga).

Tuzo ya kocha bora wa msimu ilienda kwa Kocha wa Yanga, Nasreddine Nabi.



Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA), Yessaya Mwakifulefule, akikabidhi tuzo ya TFF 2023 kwa mwakilishi wa Kocha Bora katika Ligi ya Wanawake Tanzania kutoka JKT Queens, Ally Ally. Hafla hiyo ilifanyika mkoani Tanga katika kituo cha michezo cha TFF juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mashindano ya CAF yampasua

INATOKA UKURASA 24

"Kwangu kazi nimemaliza, nimeshawapa ripoti yangu viongozi, kwa sasa kazi ipo kwa viongozi kuwapata wachezaji wote niliowaagiza viongozi wangu, naamini tutawapata na baada ya hapo kazi itakuwa kwangu na wachezaji wangu," alisema Robertinho na kuongeza;

"Simba ina jina kubwa Afrika kwa sasa, hivyo ni lazima tuwe na wachezaji wenye sifa hizo, wachezaji ambao wanaweza kukupa matokeo kwenye mechi yoyote, nikiwapata hao niliowaomba viongozi na wengine ambao ninao, tunaweza tukafanya vizuri msimu ujao na kurejesha furaha ya mashabiki wetu," alisema Robertinho.

Alisema Simba msimu huu itaanza kushiriki michuano ya 'Super League' inayoandaliwa na CAF hivyo lazima wawe na wachezaji watakaopambana na timu kubwa kama Al Ahly na Mamelod Sundown ambazo zote zitakuwapo kwenye michuano hiyo itakayohusisha timu nane.

Katika hatua nyingine, Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema wanafahamu maumivu wanayopitia mashabiki wa Simba hasa kutokana na kelele za watani zao Yanga ambao wameshinda taji la Ligi Kuu na Kombe la FA.


Ally, alisema kelele hizo za watani zao ni chachu kwao kujipanga kwa ajili ya kufanya vizuri msimu ujao kwenye michuano ya ndani na ile ya Kimataifa.

"Kiujumla kama timu hatuna cha kujivunia sana maana hatujapata tulichokihitaji msimu huu, hii inatupa nafasi ya kujipanga zaidi kwa msimu ujao, kwani ubingwa unahitaji wachezaji bora na timu imara ni jukumu letu viongozi kutafuta wachezaji sahihi na kutengeneza timu madhubuti, hilo limeshaanza kufanyika kwa umaridadi wa hali ya juu sana, hizi kelele za upande wa pili tutazijibu msimu ujao," alisema Ahmed.

# Michezo

Jumatano Juni 14, 2023

Nipashe

Vinicius Junior apewa jezi namba 7 UKURASA 22




Sehemu ya maelfu ya mashabiki wa Yanga waliojitokeza jana kuipokea timu hiyo waliporejea kutoka Tanga baada ya kutwaa ubingwa wa Kombe la FA kwenye mchezo wa fainali dhidi ya Azam FC uliochezwa Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga. Yanga ilishinda bao 1-0. **PICHA: SHUFAA LYIMO**

# Yanga yatoa msimamo wake, Mayele, Nabi

**Shufaa Lyimo na Saada Akida**

● ● ● Haipo tayari kuwauza, yafunga msimu kwa kishindo, mapokezi yatikisa Dar wakichukua kombe la FA…

UONGOZI wa klabu ya Yanga umesema haupo tayari kumuuza mshambuliaji wake Fiston Mayele na hawatamwachia kocha wao, Nasreddine Nabi, kwa kuwa bado wana uchu wa mafanikio.

**Akizungumza baada ya timu hiyo kuwasili Dar es Salaam wakitokea Tanga walipoenda kucheza mchezo wa fainali kombe la FA na kufanikiwa kulitwaa mbele ya Azam FC, Rais wa klabu hiyo, Injinia Hersi Said, alisema licha ya Mayele kubakisha mwaka mmoja kwenye mkataba wake, watakaa naye kufanya mazungumzo ya kumwongeza ili aendelee kuwapo kwenye timu hiyo.**

"Mayele bado ana mkataba na sisi mpaka msimu ujao ni mchezaji ambaye amepata mafanikio makubwa msimu huu ninaamini tutaendelea kuwa naye msimu ujao," alisema Hersi.

Alisema mashabiki wasisikilize maneno ya mtaani kuwa mshambuliaji huyo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo anataka kuondoka klabuni hapo baada ya kupata ofa kutoka klabu mbalimbali nje ya nchi.

Alisema kumekuwa na maneno mengi juu ya mshambuliaji huyo kuwa kuna ofa nyingi zimetumwa zikionyesha nia ya kumhitaji ikiwamo klabu ya Mamelodi Sundown ya Afrika Kusini jambo ambalo amelikanusha vikali.

"Nakiri kusema mpaka sasa sijapokea ofa yoyote kutoka Mamelodi Sundowns ninaomba mashabiki wetu wafuate taarifa zinazotoka kwetu, kuna maneno mengi yanasemwa mitaani na watu wenye wivu wa mafanikio yetu msimu huu, hakuna ofa yoyote na hatutamuuza Mayele," alisema Hersi mbele ya mashabiki wa timu hiyo waliofurika kuwapokea.

Aidha, alisema mbali na Mayele, pia uongozi wake unafanya mipango ya kulibakiza klabuni hapo benchi lote la ufundi lililowapa mafanikio makubwa msimu huu.

Awali baada ya mchezo wa fainali ya kombe la FA dhidi ya Azam jijini Tanga juzi, Kocha msaidizi wa timu hiyo, Cedrick Kaze alinukuliwa akisema wamemaliza kazi yao na mikataba yao imeisha rasmi siku hiyo kauli iliyoonekana kama kuwaaga mashabiki wa klabu hiyo.

Hersi ameweka wazi kuwa wameanza mazungumzo na makocha wote ili kuwasainisha mikataba mipya ya kuendelea kusalia kwenye klabu hiyo kwa msimu ujao.

Alikiri kuwa mikataba ya makocha na baadhi ya waajiriwa wao wa benchi la ufundi na wachezaji imefikia ukingoni na wako katika mipango ya kukutana nao kabla ya kwenda mapumziko kwa ajili ya kuzungumza na kuwapa mikataba mipya.

"Benchi letu la ufundi limetupa mafanikio makubwa msimu huu, uongozi tunatambua umuhimu wao, tumeanza mazungumzo tunataka wote waendelee kuwa sehemu ya kikosi chetu, Wanayanga wenzangu..., bado tuna kiu ya mafanikio, tunataka kuendelea kufanya vizuri zaidi ya msimu huu," alisema Hersi.

Kauli hiyo ya rais wa Yanga imekuja siku chache baada ya taarifa kuwa klabu ya Kaizer Chief ya Afrika Kusini imemwekea mezani mkataba mnono kocha Nabi kwa lengo la kumshawishi asaini mkataba wa kuifundisha timu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu ya Afrika Kusini.

INAENDELEA UKURASA 23

## Mashindano ya CAF yampasua kichwa Robertinho

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba, Robert Oliveira 'Robertinho', amesema mipango yake ni kuona Simba inafanya vizuri kwenye michuano ya kimataifa na sasa anaumiza kichwa kuona namna gani anakiandaa kikosi chake kwa ajili ya michuano hiyo.

Robertinho ambaye kwa sasa yupo mapumzikoni nchini kwao Brazil, amesema anataka kuona Simba inafanya vizuri msimu ujao hasa kwenye mashindano ya kimataifa na tayari ameshakabidhi ripoti yake na wachezaji anaowataka kwenye timu yake kuweza kufanya vizuri michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika watakayoshiriki msimu ujao.

"Unajua hatukuwa na msimu mzuri kwa sababu hatukuweza kuchukua ubingwa wowote na hayakuwa malengo yetu, tunahitaji kuona tunaenda mbali zaidi msimu ujao kupitia wachezaji ambao nahitaji kuwanao, nimeshwaambia viongozi wachezaji wanaotakiwa ndani ya Simba," alisema Robertinho.

Alisema ili kufika mbali kwenye mashindano ya kimataifa wanahitaji wachezaji wanaoweza kupambana na timu kubwa na kupata matokeo mazuri.

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >